SportPesa
TZS. 667,771,400
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



KESI YA MBOWE
**Shahidi** adai kumkuta mshtakiwa na bastola
UKURASA 8



**Sergio Ramos haondoki PSG**
UKURASA 23


# Nipashe

Jumanne Novemba 9, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580759
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


# TMA: Joto, ukosefu wa mvua kuendelea

UKURASA 2



Rais Samia Suluhu Hassan, akizungumza na Katibu Mtendaji wa African Leaders Malaria Alliance (ALMA), Joy Phumaphi, baada ya kuwasili Ikulu Chamwino mkoani Dodoma jana. ALMA ni taasisi ya ushirikiano wa marais 49 wa nchi za Afrika wenye lengo la kutokomeza ugonjwa wa malaria ifikapo 2030. **PICHA: IKULU**

## Serikali yaruhusu usafirishaji nje viumbe, wanyamapori

UKURASA 3



## Wanafamilia, wageni wateketea kwa moto

UKURASA 2

**MICHEZO** YANGA YAFUATA 'UBANI' KWA MLANDEGE, KMKM UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# TMA: Joto, ukosefu wa mvua kuendelea

**Na Faustine Feliciane**

MAMLAKA ya Hali ya Hewa nchini (TMA) imetaja sababu ya ongezeko la joto kwenye maeneo mengi ya nchi kuwa ni kuchelewa kwa mvua na pia jua la utosi kuwa usawa wa nchi baada ya kuvuka mstari wa Ikweta.

Akizungumzia hali hiyo, Meneja wa Kituo Kikuu cha Utabiri cha Mamlaka hiyo, Samuel Mbuya, alisema kumekuwa na ongezeko kubwa la joto kwa mikoa mingi nchini, lakini mkoa wa Dar es Salaam, Ruvuma na Kilimanjaro ikiongoza kwa kiwango cha juu zaidi cha joto.

Mbuya alisema kwa Mkoa wa Kilimanjaro hali imebadilika na kiwango cha juu cha joto kilichoripotiwa kimefika nyuzi joto 36.4 ikiwa ni ongezeko la nyuzi joto 4.6 ikilinganisha na kipindi kingine kwa mwezi huu wa Novemba.

"Pia joto limeongezeka zaidi kwa mkoa wa Dar es Salaam na kufika nyuzi 33.8 kukiwa na ongezeko la nyuzi joto 2.2 na Ruvuma limeongezeka kwa nyuzi joto 3.8 na kufika nyuzi joto 34, hali hii pia imetokea kwa mikoa mingine, tunataraji joto litaendelea kwa kipindi chote cha mwezi Novemba," alisema Mbuya.

Kadhalika, alisema wanatarajia hali itaanza kubadilika mwezi Desemba wakati jua la utosi litakuwa limeondoka maeneo ya nchi, pia mvua zitaanza kutawanyika katika baadhi ya maeneo kama utabiri uliotolewa mwezi Oktoba unavyosema.

"Nashauri wananchi kuendelea kufuatulia taarifa zetu, lakini kufuata ushauri wa kitaalamu utakaotolewa na mamlaka mbalimbali kuhusu hali hii ya kukosekana kwa mvua na kuongezeka kwa joto," alisema Mbuya.

Alisema kuwa vipindi hivyo vya joto kali nchini vitaendelea kwa kipindi chote cha mwezi Novemba na hali hiyo itaanza kubadilika mwezi ujao.

Oktoba 26, TMA ilitoa utabiri wa msimu wa mvua kwa mikoa inayopata mvua mara moja kwa mwaka ambao ulionyesha kuwapo kwa upungufu mkubwa wa mvua kwa maeneo yote yanayopata mvua hizo.

**MVUA ZA VULI**

TMA ilitabiri msimu wa mvua za vuli mwaka huu 2021 kwa maeneo yanayopata mvua mara mbili kwa mwaka Nyanda za Juu Kaskazini Mashariki, Pwani ya Kaskazini, Ukanda wa Ziwa Victoria pamoja na Kaskazini mwa Mkoa wa Kigoma.

Mkurugenzi wa Huduma za Utabiri, Dk. Hamza Kabelwa alisema, msimu wa mvua za vuli unatarajiwa kuanza kwa kusuasua katika wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Oktoba 2021 ukiwa na mtawanyiko na mwendelezo usioridhisha katika maeneo mengi. Aidha, mvua za vuli zinatarajiwa kuwa za chini ya wastani hadi wastani na zinatarajiwa kuambatana na vipindi virefu vya ukavu katika maeneo mengi yanayopata mvua za vuli.

Akizungumza kuhusu athari zinazotarajiwa kujitokeza, Dk. Kabelwa alisema upungufu wa unyevunyevu katika udongo unatarajiwa kujitokeza katika maeneo mengi, magonjwa ya mlipuko kutokana upungufu wa majisafi na salama, upungufu wa malisho na maji unaweza kujitokeza hali ambayo inaweza kuleta uwezekano wa kutokea migogoro kati ya wakulima na wafugaji.

"Matukio ya moto katika mapori na misitu yanategemewa kutokea, hivyo mamlaka husika zinashauriwa kupanga mikakati mahsusi ya kukabiliana na hali hiyo kutokana na maeneo mengi yanatarajiwa kupata mvua za chini ya wastani hadi wastani, japo izingatiwe kuwa matukio ya vipindi vifupi vya mvua kubwa yanaweza yakajitokeza katika maeneo machache," alisisitiza Dk. Kabelwa.


**UPUNGUFU MAJI**

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), mwezi uliopita iliwataarifu wananchi na wakazi wa Bagamoyo mkoani Pwani hadi Kigamboni jijini Dar es Salaam kuwapo kwa upungufu wa huduma ya maji.

Kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa na Wizara ya Maji kupitia Bonde la Wami Ruvu, kina cha maji cha Mto Ruvu kimepungua kufuatia kiangazi cha muda mrefu.

Uzalishaji wa maji umepungua kutoka lita milioni 520 kwa siku hadi kufikia lita milioni 460. Upungufu huo unatokana na kupungua kwa uzalishaji katika mtambo wa Ruvu Chini ambao husambaza maji kwa asilimia 70 ya eneo la huduma la DAWASA. Mtambo wa Ruvu Chini kwa kawaida huzalisha lita milioni 270 kwa siku na hivi sasa unazalisha kiasi cha lita milioni 210 kwa siku.

DAWASA kwa kushirikiana na Ofisi za Bonde la Wami Ruvu wanaendelea na zoezi la kusitisha matumizi ya maji kwa watumiaji wengine katika mto huo ikiwa ni pamoja kusitisha vibali vya umwagiliaji ili kuruhusu maji kufika mitamboni.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi (kulia), akimsikiliza mgeni wake Balozi wa Jamhuri ya Ireland nchini Tanzania, Mary O'Nell alipofika Ikulu jijini Zanzibar jana, kujitambulisha. **PICHA: IKULU**

# Wanafamilia, wageni wateketea kwa moto

**Na Richard Makore,**
MWANZA

WATU watano wa kaya moja wamefariki dunia kwa ajali ya moto ulioteketeza nyumba yao usiku wa kuamkia jana katika Mtaa wa Igoma Mashariki wilayani Nyamagana jijini Mwanza.

Kati ya hao, wawili walikuwa ni wageni waliotembelea kaya hiyo juzi na kulala katika nyumba hiyo.

Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji mkoani Mwanza, Ambwene Mwakibete, alithibitisha kutokea ajali hiyo.

Alisema ajali hiyo ilitokana na hitilafu ya umeme na kwamba baada ya kutokea watu hao waliokuwa wamelala katika nyumba hiyo walipoteza maisha kutokana na moshi mkali.

Alisema watu hao walifariki kutokana na moshi uliotanda katika nyumba hiyo baada ya kuwaka moto saa 6 usiku wakiwa wamelala.

Kamanda Mwakibete alisema waliopoteza maisha ni pamoja na mmiliki wa nyumba hiyo, Lameck Benedicto, mke wake, mtoto wao mmoja pamoja na watu wawili ambao walikuwa wageni katika nyumba hiyo ambao majina yao hayakufahamika.

Alisema uchunguzi wa awali umeonyesha kwamba mfumo wa umeme katika nyumba hiyo ulizidiwa na kusababisha kutokea hitilafu hiyo.

"Moshi uliwazidi marehemu na kusababisha washindwe kujiokoa kwa kutoka nje na hivyo kusababisha kukutwa na umati usiku huo," alisema.

Kamanda wa Polisi mkoani Mwanza, Ramadhan Ng'anzi, alisema moto huo ulitokea usiku wakati watu hao wakiwa wamelala.

Aliwataja waliokufa ni Lameck Bebedicto (32), Leyah Lameck (26), Yunith Lameck (1) na vijana wawili wakiume ambao majina yao hayajafahamika.

Alisema Lameck ndiye alikuwa amepanga chumba na sebule ambavyo viliwaka moto na kusababisha vifo hivyo na kwamba miili yao imehifadhiwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mwanza ya Sekou Toure.

# ...Waziri aonya athari mabadiliko tabianchi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo, amesema athari za mabadiliko ya tabianchi zinaonekana dhahiri katika maeneo mbalimbali nchini na kwamba ipo haja ya kuongeza jitihada za dhati katika kukabiliana nayo.

Jafo aliyasema hayo mjini Glasgow Scotland katika mkutano wa 26 wa nchi wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu mabadiliko ya tabianchi.

Alizitaja athari hizo kuwa ni kuongezeka kwa kina cha maji ya bahari kulikosababisha Kisiwa cha Maziwe, Wilaya ya Pangani na Kisiwa cha Fungu la Nyani, Wilaya ya Rufiji, kumezwa na maji ya bahari na kuongezeka kwa kina cha maji, kwenye Ziwa Victoria na Ziwa Tanganyika.

"Serikali imekuwa ikitumia fedha nyingi kukabiliana na athari hizi, ambazo zinatishia kurudisha nyuma juhudi za serikali za miongo kadhaa za kukuza uchumi na kuleta maendeleo kwa watu wake," Jafo alisisitiza.

Alisisitiza kuwa katika mkutano unaoendelea viongozi wa mataifa makubwa, ambayo kwa kiasi kikubwa ndio chanzo cha uzalishaji wa hewa ya ukaa wameonyesha nia ya dhati ya kutekeleza makubaliano waliojiwekea ya kutoa fedha kwa wakati, ili kutekeleza miradi ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Alisema mataifa hayo yanawajibika kutokana na makubaliano ya Mkataba wa Paris, ambao unazitaka nchi zilizoendelea kutoa Dola bilioni 100 kila mwaka kwa nchi zinazoendelea, ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

"Tunadhamiria na kusisitiza kuwa sasa tutoke kwenye maneno na twende kwenye vitendo, wenye jukumu la kutoa fedha watoe, ili miradi mbalimbali ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi iweze kutekelezeka kwa wakati," alisisitiza Jafo.

Alisema katika kuungana na Jumuiya ya Kimataifa kupunguza uzalishaji wa gesijoto, Tanzania pia imechukua hatua stahiki zikiwamo kuandaa mpango wa Taifa wa kupunguza Gesijoto (2021 - 2026), kuimarisha usimamizi wa misitu na programu za upandaji miti; kuendelea na ujenzi wa mradi wa umeme wa Bwawa la Mwalimu Nyerere, ujenzi wa reli ya kisasa, kuanza kutumika kwa gesi majumbani na kwenye uendeshaji wa mitambo viwandani na kwenye magari, badala ya dizeli na petroli na mfumo wa usafiri wa mabasi yaendayo kasi katika Jiji la Dar es Salaam, ambavyo vinachangia kupunguza uzalishaji wa hewa ukaa.

**HABARI KITAIFA**

# Serikali yaruhusu usafirishaji nje wa viumbe, wanyamapori

**Na Gwamaka Alipipi,**
DODOMA

SERIKALI imesema itarejesha biashara ya usafirishaji wa viumbe hai kwenda nje ya nchi, huku ikitoa utaratibu kwamba wanyama watakaoruhusiwa kusafirishwa ni wale waliokaushwa.

Pia imesema wanyamapori hai watakaoruhusiwa kusafirishwa ni wale walioko kwenye shughuli za utafiti na kidiplomasia.

Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja, aliyasema hayo jana bungeni wakati akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum, Mhandisi Mwanaisha Ulenge, aliyetaka kufahamu lini serikali itaruhusu usafirishaji wa viumbe hai nje ya nchi.

Mwaka 2016, serikali kupitia Waziri wa Maliasili na Utalii, Prof. Jumanne Maghembe, alitangaza kupiga marufuku biashara ya usafirishaji wa viumbe hai kwenda nje ya nchi.

Profesa Maghembe alisema serikali iliamua kuangalia upya utaratibu huo wa kuuza wanyama hai na kuamua kusitisha biashara hiyo hadi pale taratibu na misingi mizuri ya biashara hiyo itakapowekwa.

Prof. Maghembe pia aliagiza Idara ya Wanyamapori kupanga na kuweka utaratibu mpya utakaotumika kusimamia biashara hiyo pindi itakaporejeshwa tena, baada ya kumalizika kwa muda wa zuio la Serikali la miaka mitatu, ikizingatia mazingira ya uhifadhi wa wanyama hao.

Akitoa ufafanuzi wa suala hilo jana bungeni, Naibu Waziri Masanja alisema: "Serikali ilisitisha biashara ya kusafirisha wanyamapori hai nje ya nchi. Tatizo kubwa lililosababisha maamuzi hayo lilikuwa ni matokeo hasi yaliyokuwa yakiendelea kujitokeza kutokana na kufanya biashara hiyo ikiwamo kuhamisha rasilimali ya wanyamapori nje ya nchi."

Alisema Serikali ilirejesha Sh. milioni 173.28 ya ada na tozo zilizolipwa awali na wafanyabiashara kabla ya kusitishwa kwa biashara hiyo.

Alisema: "Serikali imefanya tathmini ya kina kuhusu biashara ya usafirishaji wa wanyamapori hai nje ya nchi. Kufuatia tathmini hiyo, zuio la biashara litaondolewa ambapo biashara hiyo itafanyika kwa utaratibu maalumu".

Naibu Masanja alitaja taratibu hizo kuwa ni wanyamapori hai wataruhusiwa kusafirishwa kwa shughuli za utafiti na kidiplomasia tu.

Pia alisema wanyamapori watakaosafirishwa nje ya nchi watakuwa ni wale waliokaushwa au mazao yatokanayo na wanyamapori hao.

Kadhalika, alisema biashara ya wanyamapori waliokaushwa pamoja na mazao yake itafanywa na wafanyabiashara wenye miradi ya ufugaji wanyamapori ili kuhamasisha uanzishwaji wa miradi ya ufugaji wa wanyamapori.

Alisema pia serikali itatoa muda wa miezi mitatu ili kuruhusu wafanyabiashara kusafirisha wanyamapori waliosalia kwenye mazizi na mashamba kabla ya zuio ambao walikuwa wanafugwa kwa lengo la kuwasafirisha nje ya nchi.

## Mgawo wa maji Dar waanza

**Na Frank Monyo**

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) imetangaza kuanza kwa mgawo wa maji katika Mkoa wa Dar es Salaam unaosababishwa na upungufu wa maji katika Mto Ruvu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Ofisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA, Mhandisi Cyprian Luhemeja, kutokana na hali hiyo mamlaka hiyo imeandaa utaratibu wa kuhakikisha hakuna mwananchi atakayekosa maji kutokana na kiangazi cha muda mrefu.

"Ili kuhakikisha kuwa maji kidogo yaliyopo yanafika katika mitambo ili kuchakatwa kwa ajili ya matumizi ya binadamu, timu maalum ya wataalamu wa Wizara ya Maji na DAWASA imeendelea kuhakikisha kuwa vibali vya watumiaji wengine, ikiwa ni pamoja na vya wakulima vinasitishwa pamoja na shughuli za kunywesha mifugo katika mto pia zimesitishwa," alisema Luhemeja. Alisema kuwa kwa sasa hali ya Mto Ruvu kwa majuma mawili bado iko palepale kina cha maji kiko katika mita 1.5 hadi 1.8 kwa upande wa Ruvu Juu kipo mita 16 hadi 18 na kwamba hali ya mto imeendelea kuimarika.

Alisema ya kiangazi mamlaka hiyo huzalisha lita milioni 520 kwa siku, huku yanayozalishwa sasa ni lita milioni 460 kwa siku na kwamba kuna upungufu wa asilimia 12.

Kwa mujibu wa Luhemeja hali hiyo imesababisha maji kupatikana kwa msukumo mdogo na katika maeneo mengine huduma itatolewa kwa mgawo.

"Ili kupunguza changamoto hii, DAWASA imekuwa ikitekeleza mpango wa kuhamisha maji kutoka katika vyanzo vyake vingine ikiwamo, mtambo wa Ruvu Juu, ili kuhudumia maeneo ambayo awali yalikuwa yakipata huduma kutoka katika mtambo wa Ruvu Chini. Aidha vyanzo vyake vingine vya mtambo wa mtoni pamoja na visima virefu vinaendelea kutoa huduma katika maeneo mengine ya jiji ili kupunguza changamoto iliyopo," alisema.

Aidha, alisisitiza kuwa kutokana na ukubwa wa mtandao wa DAWASA, itatoa ratiba za mgawo kwa wananchi kupitia mifumo ya kimawasiliano ya mamlaka mikoa yake ya kihuduma ili kuwafikiwa wananchi husika kwa kwa muda muafaka.

Luhemeja aliyataja maeneo ambayo hayataathirika ni Kisarawe, Chalinze, Pugu, Bagamoyo, Oysterbay, Masaki, Mikocheni, Ikulu, Hospitali ya Taifa Muhimbili, Taasisi ya Moyo ya Kikwete (JKCI) na Soko Kuu Kariakoo.



# JICA, serikali kuboresha usafiri wa reli Dar Es Salaam

**Na Elizabeth Zaya**

SHIRIKA la Maendeleo la Kimataifa la Japan (JICA), Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi na Shirika la Reli Tanzania (TRC) wamekubaliana kutekeleza mradi wa utafiti wa ukusanyaji wa taarifa na uboreshaji wa usafiri wa reli jijini Dar es Salaam kuanzia mwezi huu.

Kwa mujibu wa mwakilishi wa JICA Tanzania, Henry Kajange, utekelezaji wa mradi huo utafanyika kwa kipindi cha miezi minne na unatarajia kukamilika Februari mwaka 2022.

Kajange alisema maeneo ya utafiti na kukusanya taarifa ni miundombinu ya reli za abiria Pugu na Ubungo.

Alisema baada ya kazi hiyo kukamilika, timu iliyoundwa itatoa mapendekezo kwa ajili ya hatua mbalimbali za maboresho yake.

Alisema lengo ni kuhakikisha wanaboresha miundombinu ya usafiri katika Jiji la Dar es Salaam na kupunguza tatizo la msongamano.

"Katika mkutano wa kwanza ulioketi Novemba 4, mwaka huu, washirika wa mradi huo walipendekeza mpango wa uboreshaji wa ufuatiliaji wa uendeshaji wa reli, uwekaji ishara, usafirishaji wa bidhaa, ujenzi wa stesheni katika vituo, majengo ya biashara katika stesheni na namna bora ya kutoa huduma ya usafiri katika njia za treni za abiria zilizopo," alisema Kajange.

"Timu ya watafiti iliyoundwa, itajadiliana na maofisa wa Serikali ya Tanzania, ili kurekebisha mpango wa usafiri wa mijini wa Dar es Salaam wa mwaka 2018, uliofadhiliwa na JICA. Mpango huo ambao unakadiria kwamba jiji hilo litakuwa na zaidi ya watu milioni 10 ifikapo mwaka 2030, usafiri wa barabara pekee hautaweza kutoa uhakika na kuondoa kero ya msongamano wa magari na kutumia muda mrefu wa kusafiri ndani ya jiji hilo."

Jingine ni kupendekeza katika mkutano huo namna bora ya uboreshaji wa mfumo wa reli uliopo, kwa ajili ya maendeleo ya usafiri na mipangilio mizuri yenye uwiano.

Kwa mujibu wa Kajange, JICA inasaidia sekta ya uchukuzi kwa zaidi ya miaka 40, nchini Tanzania.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akizungumza na Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mhandisi Hamad Massauni kwenye viwanja vya Bunge jijini Dodoma, **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

# Asilimia 70 ya kesi haki za binadamu kusikilizwa

**Na Elizabeth Zaya**

MAJAJI 11 kutoka nchi wanachama wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu, imeanza kikao cha 63 cha majaji, kwa ajili ya kusikiliza mashauri 15 yaliyowasilishwa kwenye mahakama hiyo, huku asilimia 70 ya mashauri hayo yakitokea Tanzania.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kufungua kikao hicho, Rais wa Mahakama hiyo, Iman Abood, alisema kikao hicho kitafanyika kwa mwezi mmoja na kwamba Desemba 3, mwaka huu, itakuwa ndiyo siku ya kutoa hukumu kwa mashauri hayo.

Alisema majaji 11 wanatoka katika nchi za Tanzania, Congo Brazzaville, Kenya, Tunisia, Cameroon, Nigeria, Algeria, Malawi, Mali, Afrika Kusini na Rwanda.

Rais Imani aliwapongeza majaji wa Mahakama hiyo kwa mchango wao kushughulikia mashauri na kutoa maamuzi, licha ya changamoto wanazokutana nazo katika kutekeleza majukumu yao.

"Wanastahili pongezi kwa sababu pamoja na changamoto za hapa na pale ambazo wamekuwa wakikumbana nazo katika kutekeleza majukumu yao haya, lakini bado wameendelea kuwajibika, tena kwa ujasiri mkubwa kwa kila mtu na taasisi na kuhakikisha kila kitu kinakwenda sawa,"alifafanua Jaji Aboud.

"Pamoja na kwamba majaji hawa wanafahamu changamoto walizopata kutoka kwa baadhi ya nchi wanachama wakati wa utekelezaji wa majukumu yao, lakini leo tena tumewakaribisha wazungumzie maeneo chanya waliyonufaika nayo kupitia nchi hizo na wako hapa, hili ni jambo jema sana."

Pia, alishukuru kwa ushirikiano ambao mahakama hiyo imeendelea kuupata kutoka kwa nchi hizo wanachama husani nchi mbili za Niger na Gunea Bissau, ambazo zimejiunga wiki moja iliyopita.

Rais Abood aliwahakikishia majaji hao na wafanyakazi wa mahakama hiyo kuwa itaendelea kuwapo na kuendelea na shughuli zake kama kawaida, licha ya kwamba inakabiliwa na wakati mgumu kwa wadau wake kusitasita kutokana na kuwapo kwa upungufu wa rasilimali.

# Mwenyekiti wa kitongoji aua mke, ajinyonga

**Na Mary Mosha,** ROMBO

MWENYEKITI wa Kitongoji cha Urua Chini, Kijiji cha Mfuruashe wilayani Rombo, Agustine Moshi (35), amemuua mkewe, Anastasia Agustine (31) kwa kumkata na kitu chenye ncha kali na yeye kujiua kwa kujinyonga.

Mwenyekiti huyo ambaye ni mshereheshaji maarufu wilayani humo (MC), anadaiwa kutenda mauaji hayo usiku wa kuamkia Novemba 8, baada ya kusuluhishwa kwa ugomvi wa kifamilia uliowashirikisha wazazi pamoja na mke.

Mmoja wa majirani akizungumza na Nipashe, Erick Mnanda, alisema familia hiyo ilikuwa na mgogoro wa takribani mwezi moja na mke alikimbia na kwenda kuishi kwa wazazi wa mwanamume (wakwe) baada ya kupigwa na mume.

Alisema wakwe walilazimika kuingilia kati ikiwa ni pamoja na kuwashirikisha wazee katika kumaliza tatizo hilo.

"Ni siku moja baada ya kusuluhisha ugomvi, huyu baba anadaiwa kumuingilia mkewe kinyume na maumbile hali iliyosababisha mke kushtaki kwa wazazi na ndipo walipokaa chini na kusuluhisha," alidai.

Akizungumza na Nipashe, Mwenyekiti wa Ulinzi na Usalama wa Wilaya, Kanali Hamis Maiga, alisema wawili hao walikuwa na mgogoro wa kimapenzi kwa kipindi cha wiki moja iliyopita uliofika katika dawati la jinsia wilayani Rombo.

"Huyu jamaa wiki iliyopita mke wake alimpeleka dawati la jinsia hapa wilayani, walisuluhishwa lakini inaonekana halikuisha na ni suala ambalo inaonekana ni wivu wa mapenzi, wazazi nao waliingilia kati bila matokeo chanya, hivyo akaamua kuchukua jukumu la kumuua mkewe na kisha kujiua kwa kujinyonga," alisema Kanali Maiga.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Simon Maigwa, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kwamba uchunguzi wa awali umebaini kuwa chanzo cha tukio hilo ni mgogoro wa muda mrefu wa kifamilia uliosababishwa na wivu wa kimapenzi.

"Upelelezi zaidi unaendelea, miili ya marehemu imehifadhiwa katika Hospitali ya Huruma, kwa mazingira ya tukio hili natoa wito kwa jamii kutambua matatizo yetu katika familia ili kutafuta njia madhubuti zitakazoweza kutatua migogoro. Vilevile kwa wanandoa au watu walio kwenye mahusiano ya kimapenzi wahakikishe wanapata watu sahihi ndani ya familia ili kuweza kuwatatulia migogoro yao kuepuka mauaji kama hayo yaliotokea," alisema kamanda.

# TANGAZO

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA NISHATI**

**MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)**

ewura
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji
ISO 9001:2015 Certified

## MWITO WA KUTOA MAONI

***Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ni taasisi ya udhibiti wa huduma za sekta nne mchanganyiko inayojitegemea, iliyoundwa kwa Sheria ya EWURA Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania. Shughuli kuu za Mamlaka ni pamoja na kudhibiti kiufundi na kiuchumi sekta za Nishati na Maji kwa Tanzania Bara. EWURA ina wajibu wa kudhibiti shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ndogo ya Mafuta na Gesi Asili. Pia Mamlaka inadhibiti Umeme na Maji Safi na Usafi wa Mazingira kwa kuhakikisha huduma zinazodhibitiwa zinapatikana kwa viwango vya ubora wa kutosha; kwa bei halisi; salama na kwa uhakika; na kwamba watoa huduma wanapata faida halali na stahiki kwenye vitega uchumi vyao.***

Sheria ya Mafuta Na. 21 ya mwaka 2015 inaipa nguvu EWURA, kusimamia shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ya mafuta ya petroli. Kifungu cha 131 (1) cha sheria hiyo kinawataka wote wanaojihusisha na sekta tajwa kuwa na leseni iliyotolewa na EWURA.

Kutokana na kifungu cha 19(4) cha Sheria ya EWURA, Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania, taarifa inatolewa kwa umma kwamba, wafuatao wameomba leseni kujihusisha na mkondo wa chini wa sekta ya mafuta ya petroli.

| S/N | Jina la Mwombaji | Eneo | Jina la Mkurugenzi/Uraia | Aina ya Leseni |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Mosan Company Limited, S.L.P 25298, Dar es salaam. | Kiwanja Na. 2086, Eneo la Kunduchi, Wilaya ya Kinondoni, Dar es salaam. | Moshi Salum Ntankwa (Mtanzania) | Leseni ya jumla ya vilainishi |
| 2. | Hass Terminal Limited, S.L.P 78341, Dar es salaam. | Kiwanja Na. 29 na 31, Eneo la Vijibweni, Wilaya ya Kigamboni, Dar es salaam | Abdulkadir Hussein (Mtanzania) | Leseni ya jumla ya vilainishi |
| 3. | Rocktronic Limited, S.L.P. 377, Moshi. | Eneo la Ulemo, Wilaya ya Iramba, Mkoa wa Singida. | Dhiru Chauhan (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta kwa matumizi binafsi |
| 4. | Rocktronic Limited, S.L.P 377, Moshi. | Kiwanja Namba 2215, Kijiji cha Malula, Kata ya King'ori, Wilaya ya Arumeru, Mkoa wa Arusha. | Prajesh Chauhan (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta kwa matumizi binafsi |
| 5. | Rocktronic Limited, S.L.P 377, Moshi. | Kijiji cha Kiongozi, Wilaya ya Babati, Mkoa wa Manyara. | Prajesh Chauhan (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta kwa matumizi binafsi |
| 6. | M/S Tanganyika Instant Coffee Public Limited Company, Bukoba. | Kiwanja Na. 197, Kitalu "D", Bukoba Mjini, Kagera. | Rodness Milton Josephat (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta kwa matumizi binafsi |
| 7. | Ahmed Farid Bazar Petrol Station Mitundu, S.L.P. 70, Itigi, Manyoni. | Kijiji cha Mitundu, Kata ya Mitundu, Wilaya ya Manyoni, Mkoa wa Singida | Ahmed Farid Bazar (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 8. | Lake Oil Miyuji South Dodoma, S.L.P. 5055, Dar es Salaam. | Eneo la Miyuji, Kiwanja Na.1, Kitalu "BF", Dodoma Mjini, Mkoa wa Dodoma | Ally Edha Awadh (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 9. | Augustino Peter Mmasi, S.L.P 10001, Dar es salaam. | Kijiji cha Kabuku, Kata ya Kabuku, Wilaya ya Handeni, Mkoa wa Tanga. | Augustino Peter Mmasi (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 10. | Jeventina Melick Mwabena, S.L.P 91, Makambako. | Kiwanja Na. 160 Kitalu "A" Kijiji cha Ifunda, Wilaya ya Iringa Vijijini Mkoa wa Iringa. | Jeventina Melick Mwabena (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 11. | Khalid Ramadhan Hoti, S.L.P 55, Kondoa. | Kijiji Cha Kisese Dissa Wilaya ya Kondoa Mkoa wa Dodoma | Khalid Ramadhan Hoti (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 12. | Abilahi Kassim Mandepe – Rnine Gas Nyasa Petrol Station, S.L.P 27, Liwale. | Kiwanja Na. 2, Kitalu 'A', Eneo la Mtimbe – Mbamba Bay Mjini, Wilaya ya Nyasa, Mkoa wa Ruvuma | Abilahi Kassim Mandepe (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 13. | RSBG Company Limited – Nachundu Petrol Station, S.L.P 188, Tabora. | Kiwanja Na. 1017, Kitalu "F" Eneo la Iwambi, Jiji la Mbeya. | Faraja Nachundu (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 14. | Guka Filling Station Haneti, S.L.P. 174, Kondoa | Kijiji cha Haneti, Kata ya Haneti, Wilaya ya Chemba, Mkoa wa Dodoma. | Jafari Rajabu Guka (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 15. | Afroil Investment Limited-Nzega, S.L.P. 38383, Dar es Salaam. | Eneo la Nzega Mjini, Kiwanja Na.165, Kitalu "U", Mjini, Wilaya ya Nzega, Mkoa wa Tabora. | Hilmy Ahmed Mbarak (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha Mafuta |
| 16. | Valley Side Filling Station, S.L.P. 11253, Mwanza. | Kiwanja Na. 19, Kitalu "F", Uvinza Road, Eneo la Kasulu Mjini, Wilaya ya Kasulu Mkoani Kigoma. | Feisal Mukhtar Mohamed (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 17. | M & R Petroleum Company Limited, S.L.P 105003, Dar es salaam. | Kiwanja Na. 38, Kitalu "B", Eneo la Makumbusho, Wilaya ya Kinondoni, Dar es salaam. | Mohamed hamisi kamonja (Mtanzania) | Leseni ya jumla ya mafuta |
| 18. | Matemba Filling Station, S.L.P 141, Turiani. | Kijiji cha Mvomero, Wilaya ya Mvomero, Mkoa wa Morogoro. | Dickson Matemba (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 19. | Tash Oil, S.L.P 10731, Dar es salaam. | Kiwanja Na. 57, Kitalu J, Eneo la Kilindoni, Wilaya ya Mafia, Mkoa wa Pwani. | Abdulkadir Ally Quilatten (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 20. | Laulent Jackson Mabamba T/A MMG Investment, S.L.P. 491, Bukoba. | Eneo la Kilimilile, Kijiji cha Mushozi, Kata ya Kaagya, Wilaya ya Bukoba Vijijini, Mkoani Kagera. | Laulent Jackson Mabamba (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 21. | M/S Mwemage Catholic Parish, S.L.P. Private Bag, Bukoba. | Kijiji cha Itongo, Kata ya Ibwera, Wilaya ya Bukoba Vijijini, Mkoani Kagera. | Florian Mathias Kamuhabwa (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 22. | Petrolux Filling Station Kayenze, S.L.P. Mwanza. | Eneo la Kayenze, Wilaya ya Ilemela Mjini, Mkoa wa Mwanza | Chacha Maganya Magabe (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 23. | John Iganas Shewiyo, S.L.P 13619, Arusha. | Eneo la Olasiti, Kata ya Olasiti, Wilaya ya Arusha Mjini, Mkoa wa Arusha. | John Iganas Shewiyo (Mtanzania) | Leseni ya usambazaji wa Gas ya LPG |
| 24. | Rajab Zimbwe Rajab, S.L.P 69, Tanga. | Eneo la Mabawa, Kata ya Mabawa, Wilaya ya Tanga Mjini, Mkoa wa Tanga. | Rajab Zimbwe Rajab (Mtanzania) | Leseni ya usambazaji wa Gas ya LPG |
| 25. | Doreen Enterprises Ltd, S.L.P 32874, Dar es salaam. | Kiwanja Na. 1325, Kitalu "B", Ubungo Kibangu, Wilaya ya Ubungo , Dar es salaam | Steve Omari (Mtanzania) | Leseni ya usambazaji wa Gesi ya LPG |

Mtu yeyote au kikundi cha watu wenye pingamizi kwa mwombaji yeyote wa leseni hapo juu kwamba asipewe leseni, anatakiwa kuwasilisha pingamizi hilo kwa EWURA ndani ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya tangazo hili kupitia anwani tajwa hapa chini.

**Jengo la EWURA, Kiwanja Na.3, Kitalu AD, Medeli West, S.L.P 2857, Dodoma.**

**Imetolewa na:**

**Mkurugenzi Mkuu.**
**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji -EWURA**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# BoT imechelewa kwa hili, lakini...

**BENKI** Kuu ya Tanzania (BoT), imetoa taarifa kwa umma kuwa itawachukulia hatua kali za kisheria, baadhi ya wafanyakazi wa benki na taasisi za fedha wanaoshiriki ubadhirifu kupitia mikopo.

Aidha, ilibainisha matendo ovu ni kama rushwa wakati wa utoaji mikopo na kusababisha kuongezeka kwa mikopo chechefu na kutoza riba kubwa pamoja na kushirikiana na wakopaji kufanya udanganyifu.

Adhabu zilizotangazwa ni kuwafungia kuajiriwa na benki au taasisi yoyote ya fedha inayoendesha shughuli zake nchini, pia kwenye taasisi au benki inayosimamiwa na BoT.

BoT inasema utafiti uliofanywa unaonyesha ongezeko la mikopo chechefu katika sekta ya benki ni moja ya sababu kubwa ya benki na taasisi za fedha kutoza viwango vikubwa vya riba za mikopo na kuhatarisha uimara wa sekta hiyo na kuathiri uchumi wa nchi.

Katika kukabiliana na hilo, BoT imesema itaendelea kufanya ukaguzi wa benki na taasisi hizo ili kubaini sababu za kuongezeka kwa mikopo hiyo, na kwa wafanyakazi ambao watahusika moja kwa moja na mwajiri wake atatakiwa kuchukua hatua stahiki za kisheria dhidi yao.

Tunaipongeza BoT kwa hatua hii, licha ya kwamba imechelewa sana, lakini bado kuna nafasi ya kurekebisha kasoro zilizopo ambazo zilitokana na kutokuwapo ufuatiliaji wa karibu na kuchukua hatua madhubuti. Baadhi ya wafanyakazi wa benki wamedaiwa kujihusisha na kuongeza mikopo au kukopa na wateja na baadaye kuwaacha hewani ambao wamejikuta wakilipa wenyewe na mwisho kugeuka kuwa mikopo chechefu.

Wapo ambao hushirikiana na wahalifu kwa kukopesha kampuni mikopo hewa na mwisho wanaopata hasara ni benki, lakini mtandao wa wanaofanya hivyo imekuwa ngumu kushughulikiwa na sasa tunaamini uamuzi wa BoT kuweka wazi utasaidia kupunguza au kumaliza.

Pia, imekuwa vigumu kwa wateja wa kawaida kuwafikia BoT na wengi kuishia kuumizwa na taasisi au benki husika.

Tunatarajia kuona mabadiliko makubwa na utekelezaji wa agizo hilo ili kukuza sekta ya benki na kuleta mabadiliko makubwa yatakayosaidia ustawi na kupunguza au kuondoa maumivu kwa wananchi. Miaka ya hivi karibuni kulikuwa na kasi ya benki na taasisi za fedha kuuza mali za walioshindwa kulipa mikopo, huku wengine wakichukua kadi za benki za wakopaji kwa ajili ya kutoa rejesho la mkopo kila mwezi.


Ukopeshaji huo umekuwa umiza kiasi cha wanaokopesha kunufaika na waliokopa kuwa na mzigo mzito na kushindwa kulipa madeni yao. Unapokwenda kukopeshwa unakaribishwa kwa maelezo mengi mazuri na wakati mwingine kushawishiwa kuchukua mkopo mkubwa zaidi, huku ili upate fedha hizo unatakiwa kutoa rushwa kwa baadhi ya maofisa mikopo lakini bado utatakiwa kulipa pamoja na riba kubwa.

Hali hii ilikuwa ni maumivu na sasa uamuzi wa BoT kuingilia kati ni hatua muhimu katika kusaidia wananchi kutoumizwa na hata wanapoumizwa wachukue hatua gani au kwenda kwenye mamlaka gani. Pia ni muhimu kuwa na elimu endelevu kwa wananchi ili wanapofanya maamuzi ya kukopa kwenye taasisi za fedha wanajua faida na hasara za kufanya hivyo, lakini kufuatilia kwa karibu na kutangaza hatua zinazochukuliwa.

Kwa sasa vikundi vya kijamii maarufu kama VICOBA vinavyotoa mikopo kwa wanakikundi vimepata nguvu kwa kuwa mtu anaona mkopo anaopata na riba yake ni nafuu, lakini hakuna rushwa wala mbinu chafu za kumuumiza, ingawa changamoto huwa ni pale wachache wanapoamua kukimbia na fedha husika.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Jamii iamue wasichana wasikwamishwe kielimu

**SABABU** za maumbile kama ulemavu na mzunguko wa hedhi mara nyingi zimekuwa vikwazo kwa watoto kupata haki ya elimu na kwa wasichana siku za mwezi ni hali inayowarudisha nyuma kwa sababu ya kukosa taulo za kujisitiri.

Tatizo ni kubwa kwa wale wanaotoka kwenye familia duni hawa wanajikuta katika wakati mgumu hata kukatisha masomo wanapokuwa kwenye mzunguko huo wa kila mwezi.

Katika mazingira hayo ya kutohudhuria shuleni kwa sababu ya hedhi, inaweza kuathiri uwezo wao kitaaluma, hali ambayo inaweza kuweka njia panda hatima na fursa za wasichana wengi.

Hali hiyo ndiyo imeibua wadau mbalimbali wa elimu kufanya kampeni za kupata taulo za kike ili kumwezesha mwanafunzi kusoma badala ya kubaki nyumbani kisa yuko kwenye siku zake, jambo ambalo ni hali ya maumbile. Wakati kukiwa na kampeni za kuhamasisha upatikanaji wa taulo za kike, muda umefika kwa jamii kujiwekea mikakati ya kuhakikisha watoto wa kike wanaacha na utoro unaosababishwa na hali hiyo.

Viongozi wa serikali za mitaa kwenye maeneo yao, wanaweza kuweka utaratibu wa kuzitambua familia zisizo na uwezo kiuchumi ili watoto wa kike wa familia hizo wapate msaada wa taulo. Wanaweza kuchangisha fedha kutoka kila nyumba kwa ajili ya mfuko maalum wa kununua taulo za kike kwa ajili ya watoto wa kike wanaotoka katika familia hizo ili kusaidia kumaliza utoro unaotokana na hali hiyo ya kimaumbile ambayo si tatizo bali utaratibu wa mwili wa mwanamke.

Katika jamii, yapo mambo mengi ambayo watu wamekuwa wakichangia, sidhani kama ukiwekwa utaratibu huo unaweza kushindikana kuchangia fedha kwa ajili ya kununulia taulo hizo.

Ninaamini kuwa jambo hili linaweza kuwa ndani ya uwezo wa jamii kuliko kusubiri wahisani au kufanyika kwa kampeni za kuchangisha fedha kwa ajili ya kununua taulo hilo, wakati jamii ingeweza kulifanikisha.

Mabinti wengi wanashindwa kuhudhuria masomo wanapokuwa katika hedhi, wakihofia kuchafuka jambo ambalo linasababisha kudhihakiwa na wanafunzi wenzao hasa wa kiume. Juhudi zikifanyika, inaweza kuwatengenezea mazingira mazuri ya kujisitiri ikiwamo ujenzi wa vyoo vyenye vyumba maalumu wanavyovitumia kujihudumia na kujisitiri wanapokuwa katika hedhi.

Wadau wa elimu wanasema maeneo ya vijijini ambako ndipo walipo wananchi wengi, idadi ya watoto wa kike wanaojiunga na elimu ya msingi ni kubwa ikilinganishwa na wanaoendelea na sekondari.

Katika ufafanuzi wao ni kwamba, mabinti wengi hupevuka baada ya kumaliza darasa la saba na kwamba hutoka katika familia zenye uchumi duni zinazoshindwa kumudu kununua taulo hizo. Lakini suala la uelewa mdogo wa wazazi na walezi kuhusu hedhi, linatajwa kuwafanya waamini kuwa mtoto wa kike akifikia hatua ya ukubwa anakuwa tayari kuzaa, hivyo humwozesha asije kupata mimba akiwa chini ya himaya yao.

Pamoja na hayo, ninaamini kwamba, iwapo serikali ya ngazi ya mtaa itaweka utaratibu wa kutambua familia za aina hiyo na kuhamasisha uchangiaji wa fedha za kununulia taulo hizo, utoro hautakuwa na nafasi tena.

Si utoro tu bali wazazi na walezi nao wakielimishwa, wataachana na dhana kwamba mtoto wa kike akipevuka kinachofuata ni kuolewa, badala yake watatambua umuhimu wa elimu kwa wasichana.

Ikumbukwe kuwa, ni katika kipindi cha kuvunja ungo ndicho ambacho elimu inabaki kitu kipekee kinachoweza kumsaidia binti kujitambua na kutambua nafasi yake katika jamii ili kumudu changamoto za kijamii.

Ninachoamini suala la kuweka utaratibu au mikakati ya kuhakikisha jamii inachangia upatikanaji wa taulo za kike ni la msingi badala ya kutegemea wahisani na kampeni mbalimbali za kitaifa.

## Vibanda vya wamachinga Coco Beach vyaiibua NEMC

**Na Joseph Mwendapole**

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limesema halijaridhishwa na uendelezaji wa eneo la ufukwe wa Coco Beach kuwekwa vibanda vya wafanyabiashara, kwani tathmini ya athari za mazingira hazikufanyika.

NEMC imesema itawasiliana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), ili kurekebisha kasoro zilizojitokeza katika uendelezaji wa eneo hilo, kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi Mkuu wa baraza hilo, Dk. Samuel Gwamaka, alipotembelea eneo hilo kujionea athari za kimazingira kutokana na vibanda vingi vya wafanyabiashara kuwekwa eneo hilo.

Alitaja kasoro zilizoko kwenye uendelezaji huo kuwa ni pamoja na kutofanyiwa tathmini ya athari ya mazingira kwa ufanisi, kwa ajili ya kujiridhisha na usalama wa mazingira ya bahari na watu.

Alisema serikali ina nia njema kwa wafanyabiashara wadogo, lakini wakati huo inawajibika kulinda mazingira hasa ya fukwe zinazoathirika na shughuli za kibinadamu.

"Tunapoona mabadiliko kama haya hatunabudi kujiridhisha, manispaa wana haki ya kufanya maendelezo, lakini jambo kubwa utaratibu ufuatwe. Unapoleta kundi la watu sehemu kama hii, utupaji wa taka ngumu ukoje? Au mfumo wa majitaka unakuaje?" Alihoji.

Alisema sehemu kama hiyo watu wanahitaji kwenda msalani, ili kujisitiri na ndiyo sababu kila wakati NEMC inasisitiza kufanyika kwa tathmini ya athari ya mazingira, kabla ya kuanzishwa kwa mradi, ili kujiridhisha na mambo ya msingi yatakayoboresha kulinda mazingira pamoja na afya za watu.

# Wahitimu vyuo vikuu watengewa bil. 54/-

**Na Gwamaka Alipipi,**

DODOMA

KATIKA kupunguza tatizo la ukosefu wa ajira kwa wahitimu wa vyuo vikuu nchini, serikali imetenga Sh. bilioni 54 kwa ajili ya kuwawezesha wahitimu 150,000 kupata mafunzo ya uzoefu wa kazi, ikiwamo wa fani ya kilimo.

Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana na Ajira), Patrobas Katambi, aliyasema hayo jana bungeni wakati akijibu swali lililoulizwa na Mbunge wa Viti Maalum, Dk. Thea Ntara, aliyetaka kufahamu mpango wa serikali katika kuongeza ajira kwa wahitimu wa vyuo vikuu, hususani katika sekta ya kilimo.

Akitoa ufafanuzi wa swali hilo, Katambi alisema katika kuhakikisha ajira kwa wahitimu wa vyuo vikuu zinaongezeka hususani katika sekta ya kilimo, Serikali inatekeleza mipango mbalimbali.

"Ili kuhakikisha wahitimu wengi zaidi wanaendelea kuwezeshwa kuajirika na kujiajiri, kupitia Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa, Serikali imetenga shilingi bilioni 54 ili kuwawezesha wahitimu 150,000 kupata mafunzo ya uzoefu wa kazi ikiwamo fani ya kilimo," alisema Katambi.

Katambi alitaja mipango iliyowekwa na serikali kuwa ni kutoa mafunzo ya kilimo cha kisasa kupitia programu ya kukuza ujuzi nchini, kwamba vijana 12,580 katika mikoa 17 nchini, wakiwamo wahitimu wa fani ya kilimo wamepatiwa mafunzo ya kilimo cha kisasa na sasa wapo tayari kuanza biashara ya kilimo kwa kutumia teknolojia ya kitalu nyumba.

Alisema mpango mwingine ni kuwezesha wahitimu kupata uzoefu wa kazi nje ya nchi, kwamba serikali kwa kushirikiana na Ushirika wa Wahitimu wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUGECO), wamewawezesha wahitimu 703 kwenda Israel na Marekani.

Katambi alisema kati ya hao, wahitimu 311 wamerudi nchini na wamejiajiri katika maeneo mbalimbali nchini.

Alitaja mpango mwingine ni kupitia Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) na mikopo ya halmashauri, baadhi ya wahitimu waliopatiwa mafunzo nje ya nchi wamepatiwa mikopo ya Sh. milioni 170 kwa ajili ya kujiajiri katika kilimo.

Kadhalika, alisema mpango mwingine ni kupitia vituo vya uatamizi kwa wahitimu katika mikoa ya Morogoro na Pwani, wahitimu 1,000 wamepatiwa mafunzo ya uanzishaji wa shughuli za kilimo na ujasiriamali.

Mpango mwingine ni kupitia kilimo cha vizimba, kwamba wahitimu 39 wamepatiwa fursa ya kuanzisha shughuli za kilimo, kwamba kati ya hao, wahitimu 30 wamepatiwa fursa ya kushiriki katika shamba la hekari 1,500 lililoko Mvomero mkoani Morogoro.

Alisema vilevile wahitimu tisa wamepatiwa fursa ya kushiriki katika Shamba la Kahawa mkoani Songwe.



Baadhi ya abiria wanaotoka na kuingia kwenye stendi ya Magufuli iliyoko Mbezi Luis Dar es Salaam wakivuka barabara ya Morogoro bila kupita juu ya daraja la waenda kwa miguu jana, hali inayoweza kusababisha wapate ajali. **PICHA: SABATO KASIKA**

## Uelewa duni wa wananchi huduma fedha waitisha serikali

**Na Christina Mwakangale**

SERIKALI imesema Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha, utakaotumika kwa kipindi cha miaka 10, kuanzia 2020/2021 hadi 2029/2030, hautatekelezeka, iwapo wananchi wataendelea kuwa na uelewa duni, kuhusu fursa za uwezeshaji na huduma za kifedha na kuzifahamu haki zao.

Mpango huo unalenga kuongeza wigo na fursa za upatikanaji wa huduma za fedha kwa wananchi wote, ikiwamo bima, mifuko ya hifadhi ya jamii na vikundi vidogo vya kuwezeshana kifedha kama vile vikoba.

Kamishna wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha wa Wizara ya Fedha na Mipango, Dk. Charles Mwamwaja, aliyasema hayo jana katika maonyesho ya wiki ya taifa ya huduma za fedha yanayoendelea jijini Dar es Salaam.

Maonyesho hayo yanalenga kutoa elimu kwa umma kuhusu bima, benki, masoko, dhamana na mitaji pamoja na mifuko ya hifadhi ya jamii.

Alisema uelewa kuhusu masuala ya kifedha kwa Watanzania ni chini ya asilimia 50, akisema kiwango hicho kinasababisha wananchi kushindwa kufahamu kanuni, faida na mbinu za kifedha ili kukuza uchumi wao na taifa.

"Ni ngumu kuitafuta fedha lakini ni rahisi kuipoteza. Elimu ya fedha bado haijawafikia wananchi wengi, waliyonayo ni chini ya asilimia 50, hii inahatarisha ustawi wa jamii kwa sababu fedha ndiyo kila kitu katika kufanikisha mipango, mfano akiba za vikoba vikundi vidogo ni muhimu katika kusaidia mzunguko wa fedha," alisema Dk. Mwamwaja.

Alisema pia mpango wa serikali ni kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, ili kuwa na mtaala ambao utakuwa maalumu kuelimisha masuala ya kifedha tangu shuleni, akisema kwamba elimu hiyo itaongeza uelewa wa matumizi sahihi ya kifedha kidigitali.

"Sekta inayoongoza katika fedha kidigitali ni kupitia kampuni za simu za mkononi, wananchi wengi wanatumia huduma hii. Mpango wa wizara ni kuona miaka 10 ijayo Watanzania wanafikiwa na kuzifahamu huduma, fursa za uwezeshaji zilizo rasmi kwenye ukanda wetu lakini hata duniani," alibainisha Dk. Mwamwaja.

Kadhalika, alisema uelewa mdogo kuhusu masuala ya kifedha, unasababisha watu kutofahamu haki zao kwenye sekta hiyo, huku akitoa wito kwa wananchi kushiriki maonyesho ya wizara hiyo yanayofanyika kwa siku saba, yaliyoanza Novemba 7, mwaka huu, ili kupata elimu.



Mwenyekiti wa Taasisi ya Umoja wa Wakulima Wahifadhi Mazingira (UWAMAKIZI) wilayani Muheza mkoani Tanga, Twaha Rajabu Mbarouk (kulia), akitoa maelezo kwa Mkuu wa Wilaya ya Muheza, Halima Bulembo (wapili kulia), wakati wa ukaguzi wa ujenzi wa madarasa katika shule ya msingi kijiji cha Bombani juzi, taasisi hiyo imefadhili ujenzi huo kwa kushirikiana na TANGA UWASA. **NA MPIGAPICHA WETU**

KESI YA MBOWE

# Shahidi adai kumkuta mshtakiwa na bastola

**Na Kulwa Mzee**

USHAHIDI katika kesi ya ugaidi inayomkabili Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) , Freeman Mbowe na wenzake watatu uliendelea jana kwa Mrakibu wa Polisi (SP) Jumanne Malangahe, kudai kumpapasa mshtakiwa Adamu Kasekwa kuanzia kichwani, shingoni na katika mfuko wa suruali na kukuta bastola, magazine yenye risasi tatu ambayo aliichomoa na kumkabidhi Koplo Good luck.

Shahidi huyo wa nane alidai hayo Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi mbele ya Jaji Joackim Tiganga kwa kuongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Robert Kidando.

Alidai kuwa ni Mkuu wa Upelelezi Wilaya ya Arumeru na miongoni mwa majukumu yake ni kuzuia na kupeleleza uhalifu wa makosa ya jinai wilayani humo. Alidai Agosti 4, 2020 alipigiwa simu na Kamishna Msaidizi wa Polisi, Ramadhan Kingai akimwambia ajiandae kuna kazi ya kufanya Moshi.

ACP Kingai alidai kuwa aliendа ofisini kwake Arumeru akiwa na askari watano, Inspekta Mahita, Koplo Francis, Goodluck na Aziz na aliwataarifu kuwapo kwa kundi la kihalifu linaloratibiwa na Mbowe, linalotarajia kulipua vituo vya mafuta, kukata miti na kufanya maandamano yasiyo na ukomo.

Alidai walikwenda Moshi kuwatafuta wahalifu hao, lakini kwa siku hiyo hawakufanikiwa hadi Agosti 5, 2020 walipokwenda tena baada ya kupata taarifa wako Rau Madukani.

Vile vile, alidai watuhumiwa walikuwa katika grocery (duka la vinywaji), wakati wanaikaribia hawakuona watu, lakini wakati wanaingia kwenye uchochoro walisikia sauti ya Inspekta Mahita Omary akisema kaa chini, mko chini ya ulinzi na walipofika walimkuta anamalizia kuwaambia watuhumiwa kwa makosa ya kula njama na kufanya vitendo vya ugaidi.

"Afande Kingai aliniamuru kufanya upekuzi, niliwapata mashahidi huru wawili, Anitha Mtaro na Esther Nduhulu, nilitoa vitu vyangu na mifuko ya suruali kuonyesha sikuwa na kitu na kunyoosha mikono yangu, nilimwambia mtuhumiwa wa kwanza, Adamu Kasekwa asimame, aliposimama nilimwambia ageuke nyuma na anyooshe mikono juu.

"Alinitii nilianza kumpapasa kuanzia kichwani, shingoni, kifuani na nilipofika upande wa kushoto nilipitisha mkono wangu nikakuta kitu kigumu, nilipokichomoa kilikuwa ni bastola aliyoiweka kwenye mkanda wa suruali.

"Nilichomoa magazine ilikuwa na risasi tatu, nikampa Koplo Goodluck, bastola ilikuwa aina ya Luger yenye namba A5340, nilimkuta pia na kete 58 nilizohisi kuwa dawa za kulevya zikiwa zimefungwa kwenye nailoni kama karanga na simu aina ya Itel yenye line ya Halotel na Airtel.

"Nilimpekua mshtakiwa Mohammed Ling'wenya katika maungo yake nilikuta simu katika mfuko wake wa suruali aina ya Tecno, nilikuta vikaratasi mifukoni mwake vikiwa na kete 25, nilihisi dawa za kulevya, vitu vyote nilimkabidhi Goodluck," alidai SP Jumanne.

Aliendelea kudai kuwa alijaza fomu za ukamataji mali kwa washtakiwa wote, walisaini na mashahidi pia wakasaini.

Shahidi alipohojiwa kama anaweza kuitambua silaha hiyo ikitolewa alisema anaitambua kwa jina na namba zake.

Alitambua pia fomu za ukamataji mali, lakini alipoomba kutoa kama kielelezo, mawakili wa utetezi walipinga zisipokelewe kwa sababu ya makosa ya kisheria.

Wakili Nashon Nkungu alidai sheria inayonukuliwa haipo nchini, kifungu namba 38(3) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai ya mwaka 1993.

Nashon alidai mahakama haina sheria namba 38 yenye marejeo mwaka 2018 na kupinga kielelezo hicho kisipokelewe.

Wakili John Mallya pia aliunga hoja za wakili mwenzake na kuongeza kwamba hakuna mapitio ya sheria namba 38 yaliyofanyiwa marekebisho mwaka 2018.

Mallya aliunga mkono pingamizi na aliomba kielelezo hicho kisipokelewe.

Akichangia hoja Wakili Peter Kibatala, aliunga mkono pingamizi hilo na kuongeza kwamba sheria hiyo ilifanyiwa marekebisho mwaka 2019 na 2018 kama walivyonukuu katika hati ya kukamata mali.

Akijibu Wakili Kidando alidai hoja zote hazina mashiko aliomba kurejea kifungu namba 20(1)(a)(b)na (c) cha Sheria ya tafsiri ya sheria, kifungu hicho ni maalum kwa tafsiri za sheria zote. Alidai ilikuwa inatosheleza kutaja kifupi, kutaja mwaka 2018 na alikiri kifungu kinachobishaniwa namba 38 kwa mwaka huo hakikufanyiwa marekebisho isipokuwa vingine vilifanyiwa.

Kidando anadai sheria yenyewe ilifanyiwa marekebisho mwaka huo 2018 kupitia sheria namba 7 ya mwaka 2018.

Wakili Kidando alidai sheria sura ya 20 ni moja nchini na mazingira hayo kwa uhakika zaidi haiwezi kusemwa kwamba nyaraka hiyo imetengenezwa katika sheria ambayo haipo.

"Msisitizo wa mwaka 2018 kuonekana kwenye kielelezo hicho hakuna marekebisho ya mwaka huo kwenye sheria hiyo, hata kama kifungu hicho hakikuguswa lakini hakiathiri kusema marekebisho ya mwaka 2018, hoja haina mashiko," alisema Kidando.

Kidando aliomba pingamizi litupiliwe mbali halina mashiko huku upande wa utetezi ukisisitiza kupinga kielelezo hicho kupokelewa.

Pande zote zimemaliza kuwasilisha hoja kinachosubiriwa ni uamuzi wa Jaji Tiganga wa kukubaliana na hoja za kupinga kielelezo au kutupilia mbali pingamizi kisha shahidi wa nane amalizie kutoa ushahidi wake.

## Spika atoa maagizo kuvuja mitihani ya utabibu

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, ameiagiza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, kukutana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kujadiliana sababu za kuvuja kwa mitihani ya utabibu.

Amesema katika kukutana huko wajadiliane nini kifanyike ili kuhakikisha tatizo hilo halitokei tena.

Alitoa agizo hilo jana bungeni baada ya kumalizika kwa kipindi cha maswali na majibu na kumtaka Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, Stanslaus Nyongo, kuhakikisha kamati yake inakutana na uongozi wa wizara husika kujadiliana kuhusu suala hilo, kubaini tatizo na nini kifanyike.

Ndugai alisema majadiliano hayo yafanyike na kabla ya Ijumaa ya wiki hii, kamati hiyo ije na majibu hayo bungeni.

Spika Ndugai alisema: "Nimesikia mitihani imevuja, mheshimwa Nyongo (Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma ya Jamii) embu kaeni na Wizara ya Afya mjadiliane mjue sababu za kuvuja kwake na kabla ya Ijumaa mje na majibu nini kifanyike kuhusu hili."

Serikali kupitia kwa Mganga Mkuu wa Serikali, Dk. Aifello Sichwale, ilitangaza kurudiwa kwa mitihani ya utabibu ngazi ya tano ndani ya wiki sita kuanzia Novemba mosi mwaka huu, huku ikieleza mtaalamu wa afya aliyejipa sifa kwa njia ya udanganyifu ni hatari kwa afya ya wananchi.

Pia, ilitangaza kuendelea kwa uchunguzi ili kuwabaini watu/vyuo/taasisi zingine zilizojihusisha na udanganyifu huo ili kuwachukulia hatua walioshiriki katika udanganyifu huo.

Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) liliagiza kurudiwa kwa mitihani hiyo ndani ya wiki sita na itafanyika sambamba na mitihani ya marudio kwa programu zingine za afya nchi nzima.

Pia Wizara ya Afya ilitoa maelekezo kwa wakuu wa vyuo vyote vya afya nchini kuwapa taarifa wanafunzi ili wajiandae kwa ajili ya mitihani hiyo.

Baada ya kutokea taarifa za kuvuja kwa mitihani hiyo, iliundwa kamati ya uchunguzi ambayo ilibaini kuwa ilisambazwa kupitia mitandao ya kijamii na kuonekana kwenye baadhi ya namba za simu za wanafunzi zilizofanyiwa uchunguzi.

HABARI KITAIFA

# Wakulima wapewa miche ya kahawa bure

Na Shaban Njia, NGARA

CHAMA cha Msingi cha Wakulima wa zao la Kahawa (Ngara Farmes) Halmashauri ya Ngara mkoani Kagera, kimetoa miche ya zao hilo 92,500 kwa wakulima wake 7,200, ili kuongeza uzalishaji baada ya kupatikana kwa masoko ya uhakika ya ndani na nje ya Tanzania.

Meneja wa chama hicho, Zefania Munyonyela, aliyabainisha hayo jana wakati akitoa taarifa ya ugawaji wa miche hiyo mbele ya Mkuu wa Wilaya ya Ngara, Kanal Mathias Kahabi.

Alisema miche hiyo ni aina ya Robusta 57,000 na Arabika 35,500 na inatolewa bure bila malipo kutoka kwa mkulima.

Alisema wanagawa miche hiyo bure kwa wakulima kutoka vyama vya msingi (Amcos) 11 ili kuongeza uzalishaji wa zao la kahawa kutoka tani 2,400 iliyokuwa ikipatikana hadi tani 5,000, ikiwa ni pamoja na kuongeza ushuru wa halmashauri kutoka Sh. milioni 60 mpaka Sh. milioni 90.

Aidha, alisema msimu wa kilimo wa mwaka 2019/2020 walifanikiwa kugawa miche ya kahawa bure 36,962 kwa zaidi ya wakulima 20,000 na kuzalisha kilo milioni 3.9 za kahawa na kuuza kwa wateja wa ndani na nje Sh. bilioni 11.2 na kulipa ushuru halmashauri milioni 270.9 kwa kipindi cha miaka minne. Naye Mwenyekiti wa chama hicho, Davidi Bukozo, alisema msimu wa mwaka 2018/2019 walikopeshwa kiasi cha Sh. bilioni mbili na Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) na kufanikiwa kukusanya kahawa kutoka kwa wakulima na kuzipeleka sokoni hali ambayo ilifanya kulipa mkopo huo.

Bukozo alisema msimu huu wa kilimo mwaka 2021/2022 wamefanikiwa kukopa kiasi cha Sh. bilioni 1.2 kutoka TADB kwa ajili ya ununuzi wa zao hilo na kuwahudumia wakulima wake na mpaka sasa wameshareje-sha kiasi cha Sh. milioni 200 na zimebaki Sh. bilioni moja ambazo zitalipwa hivi karibuni.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya Kahabi aliwapongeza viongozi wa chama hicho kwa kutoka miche hiyo bure kwa wakulima wake hali ambayo itaongeza uzalishaji wa zao la kahawa na mapato ya ndani ya Halmashauri ya Ngara.

Aidha, aliwataka maofisa ugani kila kata ambako kunawakulima wa zao hilo kuhakikisha wanawaelimisha namna bora ya kupanda miche hiyo, ili isiharibike na kuleta tija kwa mkulima na kuhakikisha wanajikwamua kiuchumi.

Akizungumza kwa niaba ya wakulima wa kahawa, Mulishid Manisha, alisema awali walikuwa wakinunua mche mmoja kwa Sh. 200 kutoka kwa wakulima walikuwa wakizalisha hali ambayo ilikuwa ikisababisha baadhi ya wakulima kushindwa kulima zao zaidi.

Alisema msimu uliopita alipata kilo 298 za kahawa na kuuza katika chama hicho na baada ya miaka minne ijayo anatarajia kupata zaidi ya kilo 500 kutokana na kupata miche 100 bure na fedha atakazozipata atahakikisha anakidhi mahitaji ya watoto shuleni.



Naibu Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson (katikati), akikata utepe kuzindua ofisi ndogo ya Makao Makuu ya Chemba ya Wafanyabiashara wenye Viwanda na Kilimo (TCCIA) mwishoni mwa wiki jijini Dodoma. Kulia ni Rais wa TCCIA, Paul Koyi na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, David Kihenzile. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TIRA, BoT zavutiwa huduma mpya ya bima Benki ya Exim

Na Mwandishi Wetu

MAMLAKA ya Usimamizi wa Shughuli za Bima (TIRA) na Benki Kuu ya Tanzania (BoT) zimeunga mkono ushirikiano unaoshuhudiwa hivi sasa baina ya taasisi za kifedha pamoja na kampuni za bima nchini katika kutoa huduma mbalimbali za kibima.

Aidha, zimeeleza kuvutiwa na huduma mpya ya bima ijulikanayo kama "Bima Tu, Malipo Tuachie" inayotolewa kupitia Benki ya Exim Tanzania.

Wakizungumza wakati wa uzinduzi rasmi wa huduma hiyo ya "Bima Tu, Malipo Tuachie", iliyofanyika mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam, Meneja wa Leseni na Usimamizi wa mwenendo wa soko wa TIRA, Hillard Maskini na Meneja wa Usimamizi wa Taasisi za Fedha wa BoT, Nassor Omary, walisema ushirikiano huo pamoja na mambo mengine, utaongeza wigo wa kuwafikia wateja na wananchi kwa ujumla, hivyo kukuza sekta ya bima sambamba na kuboresha huduma za kibenki nchini.

Katika kutekeleza huduma hiyo mpya Benki ya Exim imeshirikiana na kampuni 10 kubwa za bima nchini ili kuwaletea wateja wake huduma bora za bima zikiwamo, Bima ya Afya, Bima ya Safari na Bima ya Maisha ambazo zote zitatolewa pamoja chini ya benki hiyo.

"Ushirikiano huu unaoendelea hivi sasa ni hatua nzuri zaidi kufikia katika historia ya utoaji wa huduma za kibima nchini. Ndio maana sisi kama wadau na wasimamizi wakubwa wa sekta hii ya bima tunazipongeza sana taasisi za kifedha ikiwamo Benki ya Exim kwa kuendelea kutunga mkono kwa kuwa kupitia ushirikiano kama huu utasaidia kuongeza urahisi wa upatikanaji wa huduma za kibima nchini," alisema Maskini aliyemwakilisha Kamishna wa TIRA, Dk. Mussa Juma.

Alisema nia ya serikali kwa sasa ni kuongeza wigo wa mtandao wa utoaji huduma za bima kwa jamii ya Watanzania ambao kwa sasa ni asilimia 28.6 tu ndio waliofikiwa na huduma hiyo.

"Hivyo basi nadiliki kusema kwamba "Bima Tu, Malipo Tuachie" ni huduma inayoshabihiana na azma ya serikali ya kupanua ushiriki wa wananchi wengi zaidi katika huduma za bima. Zaidi naamini kupitia huduma hii tutafanikiwa kuvutia Watanzania wengi kujiunga na huduma za bima kwa kuwa sasa hawatahofia suala malipo ya mkupuo kwa kuwa Exim mpo kazini leo kwa ajili ya kesho yao," alisema.

Kwa upande wake, Nassor pamoja na kupongeza ushirikiano huo, alisema BoT imekuwa ikiunga mkono huduma za Bima kupitia benki yaani Bancassurance kwa kuwa pia inaongeza tija kwa taasisi hizo katika kuwahudumia wananchi.

"Ongezeko la watumiaji wa huduma za bima nchini kupitia katika taasisi za kifedha, pamoja na faida nyingine za moja kwa moja kwa wananchi wenyewe pia ni faida kwa wadau yaani benki, mashirika ya bima na serikali. Na hiyo ndio sababu BoT tumekuwa tukivutiwa na ushirikiano wa aina hii. Hiki tunachokishuhudia leo kinatupa faraja na matumaini makubwa sana...hongereni sana," alisema Nassor aliyemwakilisha Naibu Gavana wa BoT, Dk. Bernard Kibesse.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Exim, Jafari Matundu, alisema katika kufanikisha huduma hiyo benki hiyo imekwisha waandaa vema baadhi ya wafanyakazi wake mahususi kwa ajili ya kutoa huduma kwa kushirikiana na kampuni za bima 10 ambazo zinashirikiana na benki hiyo kuendesha huduma hiyo.

"Si tu kwamba wafanyakazi wetu wamepatiwa mafunzo mahususi kufanikisha mpango huu bali pia wameidhinishwa na mamlaka husika kuwa wameiva katika kuwasaidia wateja wetu hususani katika utoaji wa elimu kuhusu huduma za bima wanazohitaji...kwa hiyo tumejipanga haswa," alisisitiza.

Akifafanua zaidi kuhusu huduma hiyo Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Bima wa benki hiyo, Melchizedeck Muro, alisema kupitia huduma hiyo Benki ya Exim itatoa mikopo itakayowawezesha malipo ya huduma za bima za aina mbalimbali kupitia kampuni 10 za bima zinazoshirikiana na benki hiyo na wakopaji wataendelea kulipa taratibu mkopo huku wakiendelea kunufaika na bima hizo.

## Viongozi vijana wasisitizwa kutenda haki

Na Beatrice Shayo

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), wilaya ya Ubungo, Lucas Mgonja, amewashauri vijana kutenda haki katika nafasi zao za uongozi kwa kufuata kanuni za maadili.

Mgonja alitoa ushauri huo mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam, wakati wa kongamano la vijana wa chama hicho tawi la Nzasa Kata ya Kimara, alieleza vijana ni muhimu kuzingatia maadili katika kazi zao badala ya kufuata utashi wao.

Mgonja alisema vijana wanaaminiwa wanapaswa kutendea haki nafasi zao kwa kuhakikisha wanafanya kazi ipasavyo.

Alisema kijana anayekuwa kiongozi ana uwezo mkubwa wa kuwasaidia vijana wenzake katika kuwaongoza na kufanya nao waaminiwe ili waweze kuajiriwa.

"Nimewaelekeza vijana namna ya kutumikia nafasi za uongozi kwa uaminifu na wanatakiwa kuitendea haki nafasi hizo na kusaidia vijana wenzao nao kuaminika na kuajiriwa au kujiajiri," alisema Mgonja.

Alisema kupitia kongamano hilo ameweza kuwapitisha katika maeneo mbalimbali, ikiwamo vijana kusimamia maadili na maelekezo ya kanuni yao ya umoja wa vijana yanayoelekezwa katika ibara ya 1 hadi 8 ya kanuni ya vijana.

"Nimewaelekeza vijana namna gani unapopewa nafasi ya uongozi wanavyotakiwa kuitendea haki ili kuweza kuwaajiri vijana wengine kuaminiwa na kuajiriwa, sio unakuwa kiongozi halafu unakuwa mbinafsi au unakuwa hutaki kushirikiana na wenzako huu sio uongozi," alisema.

Alisema amewakumbusha vijana sifa 10 za namna gani wanaweza kuwa viongozi bora katika nafasi yoyote wanayoweza kuaminiwa au kuajiriwa ikiwamo sifa ya ushirikiano, maono, uwazi, uwajibikaji, kujituma na uaminifu katika nafasi hizo.

Aidha, aliwataka vijana kutumia simu janja katika kujipatia kipato na sio kutumia simu kwa mambo mengine. "Tumieni fursa ya dunia kuwa kwenye kiganja ili kujipatia pesa katika fursa za kiuchumi badala ya kutumia kwa mambo ambayo hayana msingi," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana tawi la Nzasa Kata ya Kimara, Hamad Zongo, alisema kongamano hilo limewahusisha viongozi vijana ngazi ya mashina, tawi, kata na ngazi za juu kwa ajili ya kupata elimu ya uongozi.

Alisema lengo kuu la kongamano hilo ni kwa ajili ya kuwapatia miiko na miongozo ya uongozi kwani vijana wengi wananafsi ya uongozi, lakini miiko ya uongozi huo wao hawafahamu.

Alisema takribani za vijana waliohudhuria kongamano hilo ni 140 ambao wamejiorodhesha katika kushiriki kongamano hilo.

# Bil. 38.15/- kukamilisha maboma 758 ya zahanati

SERIKALI imesema katika mwaka wa fedha 2021/22, Sh. bilioni 38.15 zimetengwa kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma ya zahanati 758 nchini.

Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Festo Dugange, alibainisha hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Buyungu (CCM), Aloyce Kamamba.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji mpango wa serikali wa kujenga zahanati na vituo vya afya katika Wilaya ya Kakonko.

Akijibu swali hilo, Dk. Dugange alisema serikali inaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa zahanati na vituo vya afya vya kimkakati nchini.

Alisema Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko imetengewa Sh. milioni 150 kwa ajili ya ukamilishaji wa zahanati tatu.

"Katika mwaka wa fedha 2021/22 serikali imetoa fedha za makato ya tozo za miamala ya simu Sh.bilioni 55.25 kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya 221 kwenye tarafa zisizo na vituo vya afya vyenye uwezo wa kutoa huduma ya upasuaji, ambapo Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko imepokea Sh.milioni 250 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya katika Tarafa ya Nyaronga kata ya Gwalama," alisema.

Hata hivyo, alisema mpango wa serikali ni kuendelea kujenga zahanati na vituo vya afya katika Wilaya ya Kakonko na nchini kote katika maeneo ya kimkakati kulingana na vigezo vilivyowekwa badala ya kila kijiji na kata.

Alifafanua serikali inaendelea kujenga hospitali, vituo vya afya na kukamilisha ujenzi wa maboma ya zahanati nchini kwa kadri fedha zinavyopatikana.

"Katika mwaka wa fedha 2020/21 Serikali imetoa fedha Sh. bilioni 27.75 kwa ajili ya ukamilishajiwa maboma ya zahanati 555, Sh. bilioni 32.34 kwa ajili ujenzi wa wodi tatu kwenye hospitali 67 na Sh. bilioni 27 zimetolewa kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa hospitali 27," alisema.

Aidha, alisema Sh. bilioni 34 zimetolewa kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba kwenye hospitali 67 za awamu ya kwanza ya ujenzi.

Pia alisema serikali pia imetoa fedha Sh. bilioni 35.7 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa vituo vya afya 83.



Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, wakiwa katika kikao cha kamati bungeni jijini Dodoma, kamati hiyo ilikutana na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kujadili utendaji wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA). **PICHA: BUNGE**

# Pride yawekwa kwenye hatua za ufilisi

WIZARA ya Fedha na Mipango, imesema Kampuni ya Pride ipo kwenye hatua za ufilisi baada ya Ofisi ya Msajili wa Hazina kuagizwa kusimamia suala hilo.

Aidha, madai yoyote yanayohusu kampuni hiyo yatashughulikiwa kwa kufuata taratibu za ufilisi.

Naibu Waziri, Hamad Yusuf Masauni, aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Mtwara Mjini (CCM), Hassan Mtenga.

Katika swali lake, Mtenga alihoji lini serikali itashughulikia urejeshwaji wa fedha za wananchi wa Jimbo la Mtwara Mjini ambao walijiunga na Pride kwa ajili ya kupata mkopo.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Masauni alisema kulikuwa na shauri mahakamani lililofunguliwa mwaka 2016 kuhusu umiliki wa kampuni ya Pride.

"Baada ya kukamilika kwa shauri hilo na kutolewa hukumu tarehe 11 Novemba, 2018 kuwa kampuni ya Pride Tanzania ni mali ya serikali," alisema.

Hata hivyo, alisema serikali ilifanya tathmini ya hali ya kampuni na kufuatiwa na ukaguzi maalum uliofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kutambua mali na madeni ya kampuni hiyo ambapo taarifa ilionyesha kuwa kampuni ina madeni makubwa kuliko mali zilizopo.

## Serikali yafafanua ufutaji mashamba yaliyotelekezwa

BUNGE limeelezwa kuwa ufutaji wa mashamba yaliyotelekezwa nchini ni zoezi endelevu kwa ajili ya kulinda maslahi mapana ya taifa, wananchi na wawekezaji.

Pia hatua hiyo inalenga kupunguza migogoro ya matumizi ya ardhi ambayo imekuwa ikijitokeza katika maeneo mbalimbali nchini.

Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Angelina Mabula, alitoa kauli hiyo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Korogwe Vijijini (CCM), Timotheo Mnzava.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji lini serikali italifuta Shamba la Mwakinyumbi Estate lililotelekezwa kwa muda mrefu na kuwapa wananchi wa Hale na maeneo jirani ili kufanya shughuli za kiuchumi.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri huyo alisema shamba la Mwakinyumbi Estate lilimilikishwa kwa barua ya toleo yenye kumbukumbu namba TRKF/76/65/AOM kwa muda wa miaka 99 toka tarehe 1 Aprili, 1989 kwa matumizi ya kilimo.

Alisema mmiliki alipewa masharti ya umiliki kwa mujibu wa Sheria za Ardhi ambapo miongoni mwa masharti hayo ni uendelezaji wa shamba na ulipaji wa kodi ya pango la ardhi kila mwaka.

"Ukaguzi uliofanyika uwandani umebaini kuwa shamba tajwa limetelekezwa na hakuna uendelezaji wowote uliofanyika na kwa sasa shamba hilo linadaiwa kiasi cha Sh. milioni 174.073 ikiwa ni kodi pamoja na malimbikizo kwa muda wa miaka 17 kuanzia mwaka 2005 mpaka 2021," alisema.

Kutokana na hali hiyo, alisema serikali ilianza kuchukua hatua za kisheria za kubatilisha miliki ya shamba husika kwa kutuma ilani ya kusudio la ubatilisho wa miliki ya siku 90.

Alisema mmiliki hakuwasilisha utetezi wowote juu ya ilani ya ubatilisho aliyotumiwa kufuatia uvunjaji wa masharti kama ilivyoainishwa katika barua yake ya toleo, hivyo serikali inaendelea na hatua za ubatilisho.




Habari zote na Augusta Njoji

Nipashe
TESA
Jumanne Novemba 9, 2021
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI



Ukurasa 14

## Mwongozo chakula na lishe shuleni, umma uelimishwe hasa umuhimu wake



Ukurasa 12

## WAHITIMU MSIKIE

Msisubiri ajira rasmi angalieni ni wapi ujuzi wenu unatumika kwa ufanisi zaidi, jitoleeni

SAYANSI

NA GAUDENSIA MNGUMI

# Mkutano tabianchi ukomeshe ukataji miti 'Bongo' 2030

WIKI iliyopita mataifa mbalimbali yamekutana jijini Glasgow Scotland, kwenye mkutano wa kutibu dunia, unaoweka mikakati ya kujinusuru kutokana na uharibifu mkubwa wa mazingira unaosababisha mabadiliko ya tabianchi na kuongeza kitisho cha dunia na viumbe kuangamia.

Mkutano wa mabadiliko ya tabia na kupunguza joto duniani COP26 au 'Conference of the Parties' mwaka huu umeibuka na azimio la kuokoa 'mapafu ya dunia' na kukomesha ukataji miti ifikapo 2030.

Hii ni misitu inayosafisha hewa chafu ya ukaa na kuzalisha ya oksejini inayotumiwa na kila kiumbe hai pamoja na wanadamu.

Uharibifu wa mazingira unaotokana na kukata miti umeongeza joto duniani, kuyeyusha theluji inayojaza bahari, kuongeza joto linaloua watu na viumbe, kusababisha vimbunga, mafuriko, kuibuka magonjwa na kutishia uhai wa viumbe bahari wanaokufa kwa kukosa hewa safi na kuzidiwa na joto.

Huko Glasgow wakuu wa nchi walioshiriki wamekubaliana kuikoa na kurejesha misitu ya dunia katika ubora wake ili kuiwezesha dunia kupumua ikimaanisha kusafisha hewa chafu na kutoa nyingine safi ya oksjeni ni kwa mujibu wa Mtandao wa UN News.

Azimio la mkutano wa Viongozi wa Dunia wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi au COP26, pamoja na makubaliano hayo ya viongozi wanaambatanisha ahadi kutoka kwa watendaji wa sekta za umma na binafsi kupambana na mabadiliko ya tabianchi, kukabiliana na uharibifu wa viumbe hai na janga la njaa huku wakilinda haki za watu wa jamii za asili.



Rais Samia Suluhu Hassan, akihutubia Mkutano wa Wakuu wa Nchi wa Mabadiliko ya Tabianchi nchini Scotland. **PICHA: MTANDAO**

Makubaliano hayo yanatiwa saini na viongozi wanaojikita katika masuala ya misitu na matumizi ya ardhi na kutaka kusitisha na kubadili mwelekeo wa ukataji miti katika muongo ujao kama sehemu ya mkakati ya kupunguza gesi chafu za viwandani.

"Leo itakuwa siku ya ukumbusho, tunaandaa mwongozo wa jinsi tunavyoweza kuhifadhi mapafu ya ulimwengu," anasema Sandrine Dixson-Declève, akiwakaribisha washiriki mkutano wa COP26, uliofanyika Glasgow Scotland.

### BONDE LA CONGO

Tamko la kulinda mapafu ya dunia yanalizungumzia Bonde la Congo. Ulinzi wa misiti ya Ikweta ya Congo umetiwa saini na zaidi ya nchi 10. Mfuko wa Kimataifa wa Bezos na Umoja wa Ulaya (EU) zinaahidi kukusanya dola bilioni 1.5 kulinda misitu, maeneo oevu na sehemu nyingine muhimu zinazochangia kuzalishwa hewa ya oksjeni.

"Bonde la Congo ni moyo na mapafu ya bara la Afrika, hatuwezi kushinda vita dhidi ya mabadiliko ya tabianchi ikiwa hatutalishikilia bonde hilo," anasema Rais wa Gabon, Ali Bongo Ondimba.

Kwa mujibu wa Waziri Mkuu wa Uingereza, Borris Johnson, mpango huo pia ni sehemu ya ahadi mpya ya kimataifa ya ufadhili wa misitu ya zaidi ya dola bilioni 12.

"Ahadi kubwa zaidi za pamoja ya fedha za umma kukusanywa kwa hatua kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi katika historia. Hebu tukomeshe maangamizi haya makubwa ya kimataifa yanayofanywa kwa kutumia msumeno unaomaliza mabilioni ya miti duniani," ananukuliwa na UN News.

### AZIMIO GLASGOW

Katika tamko hilo la COP 26, viongozi wanaahidi kuimarisha juhudi za pamoja za kuhifadhi misitu na mifumo mingine ya ikolojia ya nchi kavu na kuharakisha urejeshwaji wake, pamoja na kuwezesha sera endelevu za biashara na maendeleo, kimataifa na kitaifa.

Azimio pia linataja uwezeshaji wa jumuiya za wenyeji, ikiwa ni pamoja na watu wa kiasili, ambao mara nyingi huathiriwa vibaya na unyonyaji na uharibifu wa misitu.

Azimio linalenga vilevile kutekeleza na kubuni upya sera na programu za kilimo ili kupunguza njaa na kunufaisha mazingira.

Fedha pia ni muhimu katika ahadi hiyo, ikiwa viongozi wameahidi kuwezesha upatikanaji wa fedha na malengo ya kimataifa ya kubadili upotevu na uharibifu wa misitu, huu ni wakati wa kuhakikisha sera za kuharakisha hatua za mpito kwa ajili ya uchumi wa kijani.

Katika muongo uliopita, fedha ziliingia katika matumizi mabaya ya ardhi badala ya ulinzi wa misitu, uhifadhi na kilimo endelevu.

Ahadi imetiwa saini pia na zaidi ya taasisi 30 za kifedha zinazohodhi zaidi ya dola trilioni 8.7 ya mali ya kimataifa chini ya usimamizi wake, zikilenga kubadilisha hilo.

Zinataja pia kuondokana na mipango inayowekeza katika minyororo ya ugavi wa bidhaa za kilimo zenye hatari kubwa ya ukataji miti na kuelekea katika kukuza uzalishaji endelevu.

Taarifa za BBC zinakariri Ripoti ya 'Global Forest watch' inayoonyesha kuwa misitu mikubwa ya kitropiki inapitia wakati mgumu duniani kuanzia Amazon huko Amerika Kusini, Congo, Afrika ya Kati na Kaskazini hadi Indonesia.

Misitu ya Amazon ni eneo la makazi ya watu takribani milioni 20 na ni sehemu ambayo dunia inapumua sehemu hiyo ikitunzwa na makabila mbalimbali yanayoishi katika eneo lililotengwa.

Pamoja na kutoa chakula na makazi, miti katika eneo hili ni muhimu duniani ili kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi. Lakini mamilioni ya hekta za misitu imekuwa ikipotea miaka ya hivi karibuni kutokana na shughuli za kibiashara na kilimo inasema BBC.

Takwimu za mwaka 2018 zinaonyesha kuwa kuna utofauti kati ya upungufu mkubwa wa misitu kwa miaka miwili iliyopita huku miti mingi ikiwa imepotea kutokana na kuchomwa moto, kwa mujibu wa BBC.

Dunia inaitegemea misitu ya Amazon na Afrika mapafu yako kwenye misitu ya Congo, ambayo ni nchi ya pili duniani kwa kupoteza misitu huku Colombia, Bolivia na Peru pia kukiwa na ongezeko kubwa la kupotea kwa misitu asilia.

### MAPAFU YA TANZANIA

MIsitu asilia ni muhimu hii haipandwi na binadamu au kuhudumiwa kwa namna yoyote, ni ile iliyoota yenyewe. Ni misitu ya zamani na hii inatajwa na wataalamu kuwa ina uwezo wa kutunza hewa ukaa,

INAENDELEA UK.12

ELIMU
NA GWAMAKA ALIPIPI

WAHITIMU MSIKIE

# Msisubiri ajira rasmi angalieni ni wapi ujuzi wenu unatumika kwa ufanisi zaidi, jitoleeni

TATIZO la kukosekana ajira rasmi linazidi kuongezeka na kinachoonekana ni uwezo mdogo wa Watanzania hususani wahitimu wa vyuo vikuu ambao licha ya kuelimika wanashindwa kujianzishia ajira zenye tija kumudu maisha yao.

Kuwapo kwa hali hiyo, kunamsukuma Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Profesa William Anangisye, kwenye mahafali ya 51, yaliyofanyika Oktoba mwaka huu, akiwataka vijana UDSM na wengine kujiibulia fursa.

Anawakanya wasisubiri ajira rasmi serikalini au kwenye sekta binafsi, bali wawe wepesi kuangalia ni wapi ujuzi walioupata vyuoni unaweza kutumika kwa ufanisi zaidi, hata ikiwezekana wafanye kazi za kujitolea kuutambulisha na kuuendeleza.

Profesa Anangisye anasema kwa kufanya hivyo wahitimu wa vyuo vikuu watajenga kujiamini, ujuzi na mchango wao utatambuliwa na kuinufaisha jamii.

“Tumieni elimu yenu kama ushawishi kwa wengine ili muwe chachu ya mabadiliko katika jamii yetu. Kumbukeni kuwa elimu na maarifa mliyoyapata ni mali ya umma na haviwezi kuwa chachu ya mabadiliko yaliyokusudiwa kama haitatumika katika kutatua matatizo ya Watanzania,” anasema Makamu Mkuu wa Chuo.

Kadhalika, anawataka wahitimu wa vyuo vikuu wanapojiunga na jamii kama sehemu ya nguvukazi wawe wepesi wa kujifunza mambo mapya na kubadilika kwa haraka, ili wasiachwe na wakati.

Profesa Anangisye anasema: “Jitahidini kudumisha sifa ya UDSM popote mtakapokuwa, kwa kuwa chachu ya maendeleo na mifano ya kuigwa na wengine. Kamwe msishushe hadhi ya chuo kwa kufanya jambo lolote lisilofanana na sifa na umaarufu wake.”

Kadhalika, anawataka wahitimu hao kuwa watu wa kutafuta fursa badala ya kusubiri ziwafuate, akisema kuwa jambo hilo siyo rahisi kutokea katika dunia ya leo.



Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Profesa William Anangisye. **PICHA: MTANDAO**

Aidha, anawaambia wahitimu hao kuwa na hulka ya kuthubutu kufanya mambo ambayo yanaonekana ni magumu, na kwamba hata pale watakaposhindwa kufikia mafanikio yao wasife moyo.

“Mnapokwenda mtaani mwendelee kuchukua tahadhari zote za ugonjwa COVID-19 sambamba na kupata chanjo ya kujikinga na ugonjwa huo kwani bado upo na unaleta madhara katika jamii,” anakumbusha Prof. Anangisye.

Anawataka wanafunzi hao kutafuta fursa badala ya kusubiri fursa ziwafuate, jambo ambalo si rahisi kutokea leo.

“Mtakapokuwa mnatekeleza wajibu wenu wa kujitafutia maisha mazuri na kuendeleza nchi yetu, muwe na uthubutu na kujaribu mambo ambayo yanaonekana ni magumu.

“Hata pale mtakaposhindwa kufikia mafanikio mliyotarajia, msife moyo, bali endeleeni kuwa na ari ya kujaribu tena na tena hadi mafanikio yapatikane,” anasema Prof. Anangisye.

> “Tumieni elimu yenu kama ushawishi kwa wengine ili muwe chachu ya mabadiliko katika jamii yetu. Kumbukeni kuwa elimu na maarifa mliyoyapata ni mali ya umma na haviwezi kuwa chachu ya mabadiliko yaliyokusudiwa kama haitatumika katika kutatua matatizo ya Watanzania,” anasema Makamu Mkuu wa Chuo.

Anasema katika mahafali hayo duru ya pili na ya tatu wanafunzi 4,298 wamehitimu na kutunukiwa shahada, stashahada na astashahada mbalimbali.

Anasema wahitimu hao ni kutoka katika ndaki (vitivo vya ) Uhandisi na Teknolojia, Teknolojia za Habari na Mawasiliano, Shule Kuu za: Biashara, Sayansi za Kilimo na Teknolojia ya Chakula; Sayansi Asilia na Tumizi; Sayansi za Jamii Madini na Jiosayansi.

Wengine ni kutoka Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Shule Kuu za Uchumi, Sayansi ya Akua na Teknolojia ya Uvuvi, Sheria, Uandishi wa Habari na Mawasiliano ya Umma (SJMC) na Taasisi ya Taaluma za Maendeleo (IDS).

Mwenyekiti wa Baraza la UDSM, Jaji Damian Lubuva, anawataka wahitimu hao kwenda kutumia ujuzi walioupata, kujifunza na kushirikiana na jamii.

Anasema: “Mazingira ya sasa ni tofauti na miaka ya nyuma, wakati sisi tunasoma tulikuwa tumeshaandaliwa ajira, lakini kwa miaka ya sasa ni lazima utafute ajira, lakini msisubiri kuajiriwa, tumieni ujuzi wenu kujiajiri”.

Jaji Lububa pia anawataka wahitimu hao kwenda kuwa mabalozi wazuri wa UDSM katika jamii, sambamba na kuendelea kuchukua tahadhari ya magonjwa ya mlipuko.

**USAWA KIJINSIA**

Mkuu wa UDSM, mstaafu Jakaya Kikwete, kwenye mahafali hayo anasema usawa wa kijinsia unapiga hatua katika ngazi ya elimu ya juu nchini.

Anasema takwimu zinaonyesha kuna mafanikio katika kuelekea usawa kwa kiwango cha 50 kwa 50 unaanza kuonekana.

Anasema hilo linaonekana kwenye takwimu na kwamba kati ya wanafunzi 4,121 waliohitimu elimu ya juu UDSM, wanaume ni 2,201 na wanawake ni 1,920 ambao ni sawa na asilimia 46.6.

Mkuu wa Chuo anabainisha kuwa idadi ya wanawake wanaomaliza vyuo vikuu inaendelea kuongezeka.

Rais Mstaafu Kikwete anasema: “Takwimu hizi zisipoelezwa hutuwezi kujua kama tunapiga hatua kubwa sana kwenye usawa wa kijinsia hadi ngazi ya elimu ya juu ambako wanafunzi wengi wa kike walikuwa hawafiki au kumaliza. Leo mambo yanabadilika.”

Anasema ngazi ya elimu ya msingi wanachukua wanafunzi 50 kwa 50 kwa sababu wanaandikishwa kwa usawa wa kijinsia.

“Wanapoanza kidato cha kwanza waanza wote lakini kadri muda unavyokwenda wanapungua sijui inakuwaje? Huku ngazi ya chuo kikuu wanakuwa wachache. Lakini sasa tunaelekea hatua ya 50 /50 kwenye suala la jinsia katika elimu ya juu,” anasema Mkuu wa Chuo Kikwete.

# Mkutano tabianchi ukomeshe ukataji miti ‘Bongo’ 2030

**INATOKA UK.11**

ndio maana upoteaji wa milioni ya hekta za misitu ya asili siyo jambo la kuvumiliwa tena.

Kazi iliyoko sasa ni Tanzania kulinda hifadhi za miti ya asili kama inavyoelekezwa na mkutano wa COP26.

Ulinzi unahitajika katika Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro, Amani, Chome, Kilombero, Magamba, Milima ya Rungwe, Milima ya Uluguru na Udzungwa. Maeneo haya ni muhimu kupata mvua, hewa safi na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa taifa hili.

Lakini, baharini nako hali si shwari kuna baadhi ya vijiji vimezama, kutokana ongezeko la kina cha bahari chanzo kikihusishwa na ukataji wa mikoko na uharibifu wa mazingira bahari na kuharibu matumbawe.

Kwa mfano Pemba sehemu za makazi zimezama na bahari, chumvi kuongezeka kwenye ardhi na kukwamisha kilimo huku mawimbi makubwa ya bahari yakitishia ustawi wa watu na uzalishaji.

Maeneo ya Msuke, Kisiwa cha Panza na Mtamwe Juu Kisiwani Pemba ni sehemu zenye changamoto hizo. Kwa upande mwingine Kijiji cha Mdimni kilichoko mkoani Pwani kimezama baharini baada ya kukivamiwa na mawimbi na maji bahari.

Yote hayo ni mabadiliko ya tabia yanayochochewa na kukata mikoko ambayo ni maalumu kukata kasi ya mawimbi na dhoruba za baharini. Aidha kuchota mchanga maeneo ya ufukweni nako kunaongeza mashimbo na kusababisha maji kujaa na kuvamia makazi.

Ni vyema kampeni za kitaifa zikaanza nyumba kwa nyumba kijiji kwa kijiji kuhimiza Watanzania kutunza misitu. Watu wahimizwe kufahamu kuwa misitu ya asili ni muhimu kupunguza joto, kuondoa hewa ukaa na kurekebisha mifumo ya kiikolojia ardhini.

Leo dunia inatajwa kuwa kuna ongezeko la joto la kiwango cha deigrii 1.2 zaidi kuliko ilivyokuwa karne ya 19 (miaka ya 1,800), wakati kiwango cha hewa ukaa kilichojaa angani ni zaidi ya asilimia 50 jambo linalohatarisha maisha ya binadamu na viumbe hai vingine.

ELIMU
NA SABATO KASIKA

# Waziri marufuku uhamisho anapokelewa kwa mtazamo huu

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) Ummy Mwalimu, ametangaza marufuku ya uhamisho wa watumishi walio chini ya wizara yake kutoka vijijini kwenda mjini, akisema kutaka kuvikimbia vijiji na kuishi mijini ni miongoni mwa mambo yanamkera.

Marufuku hiyo inawagusa hasa wale wanaotaka kwenda katika majiji na manispaa, huku akiacha milango wazi kwa watumishi wanaopenda kuondoka maeneo hayo kwenda halmashauri za vijiji akihimiza waharakishiwe uhamisho.

Anatangaza marufuku hiyo mwishoni mwa mwezi uliopita alipokuwa akitaja mambo makubwa mawili ambayo yanamkera ndani ya TAMISEMI, akifafanua hakuna uhamisho mpaka atakapotangaza tena, na kwamba watumishi wa mijini wanaotaka kwenda vijijini waharakishiwe uhamisho lakini wa vijijini kwenda mjini, hapana.

Nipashe inazungumza na baadhi ya wadau wa elimu ili kupata maoni yao jinsi wanavyouchukulia uamuzi huo, ikianza na Katibu Mkuu wa Chama cha Kuetea Maslahi na Haki za Walimu Tanzania (CHAKAMWATA), Meshack Kapange, anayesema kuna haja ya kutafakari zaidi.

Anasema anamshauri waziri kuangalia kwa kina uamuzi huo, kwa maelezo kuwa kila mtumishi ana haki ya kuhama bila kuvunja sheria na suala la mfanyakazi kwenda sehemu yoyote kuendelea na utumishi wa umma liko kisheria.

Anafafanua kuwa, hakuna sheria ya kupiga marufuku kama ambavyo amefanya na kuongeza: "Kuna sababu mbalimbali zinazomfanya mtumishi wa umma kuhama sehemu moja kwenda nyingine, ziko za kimaumbile, afya, kiuchumi, ndoa na hata kutunza wazazi," anasema Kapange.




Wanafunzi wakimsikiliza mwalimu (hayupo pichani) akifundisha. Mazingira bora ya kufundishia ni kivutio kwa walimu kupenda kazi bila kujali wako kijijini au mjini. **PICHA: MTANDAO**

Katibu anasema, kumekuwapo na wimbi kubwa la watumishi kutaka kutoka vijijini kwenda mijini, na kwamba wana haki ya kufanya hivyo, akidai mazingira huko si rafiki kwao.

"Njia ambayo itasaidia kumaliza tatizo hili la walimu kutaka kutoka vijijini, ni serikali kuboresha mazingira ya huko na wapewe posho ya mazingira magumu ili angalau wawe na ahueni badala ya kupiga marufuku," anashauri.

Mwalimu huyo anasema, hayo yakifanyika, kasi ya kuomba uhamisho inaweza kupungua, kwa kuwa mazingira duni ndiyo chanzo kikuu cha walimu kutamani kukimbilia katika shule za mijini.

"Ujenzi wa nyumba za walimu nalo ni jambo linalotakiwa kupewa mkazo na pia kuwapo kwa huduma muhimu kama kivituo kwa walimu kutotamani kukimbilia mijini," anasema.

**SENSA KWANZA**

Rais mstaafu wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT), Gratian Mkoba, anaunga mkono uamuzi wa waziri, lakini anatoa ushauri kwamba afanye sensa ya wanaotaka uhamisho kwanza ili marufuku ifanye kazi vizuri.

Anasema, wapo baadhi ya walimu katika shule za mijini, hawana sababu za kuhamia vijijini na pia wapo wa vijijini, wana sababu za kuwafanya wahamie mijini, na kwamba ikifanyika sensa watajulikana.

"Kwa mfano walimu hawajaolewa au hawajaoa, wanafundisha mijini, hao wangehamishiwa shule za vijijini, lakini wapo wameolewa wanafundisha vijijini, waume zao wako mijini, hao ni vyema wangeruhusiwa kuhama wawafuate wenzi wao," anasema Mkoba.

Aidha, anasema shule nyingi za vijijini zinakosa walimu kwa sababu zinazoweza kuzuilika, na kushauri kuwa pamoja na marufuku ya waziri, kuna haja ya kufuatilia vikwazo vinavyochangia tatizo hilo.

"Niliwahi kwenda shule moja ya msingi huko Mkuranga mkoa wa Pwani nikakuta ina walimu watatu, hao wanaweza kijigawaje ili wafundishe darasa la kwanza hadi la saba? Hapo hakuna kusoma," anasema.

Mwalimu huyo mstaafu anasema, katika mazingira hayo ya wanafunzi kukosa vipindi vingi vya masomo, wanaletewa mtihani wa darasa, ili waufanye huku wakiwa hawajaandaliwa vizuri.

"Kuna ujanja hufanyika unaosababisha walimu wasio na sababu za kufundisha shule za mijini kutohamia vijijini, nimuombe waziri afuatilie sana atazijua kile ninachokisema ili uhamisho uendelee kufanyika mjini na vijijini," anasema.

**BUSARA ITUMIKE**

Mwenyekiti wa Taasisi ya Utawala Bora na Maendeleo Tanzania (CEGODETA), Thomas Ngawaiya, anashauri busara itumike kwa ajili ya kufanikisha marufuku hiyo ya waziri.

Anasema kuna njia zinazoweza kutumika ili kupunguza wingi wa walimu wanaotamani kukimbia kutoka vijijini kuhamia shule za mijini, ikiwamo kuwapa mishahara mikubwa na posho nzuri walimu wa vijijini.

"Hatua hiyo inaweza kushawishi walimu kutohama vijijini au kukimbilia shule za vijijini, kutokana na kwamba watakuwa wanapata maslahi makubwa kuliko wenzao wa mijini," anasema Ngawaiya.

Ngawaiya anasema, hivyo ni vinaweza kuwa vivutio vikubwa kwa walimu, ili waweze kufanya kazi yao kwa ufanisi kuliko kuwapo kwa manung'uniko miongoni mwao huku wakitamani kuhamia shule za mijini.

"Busara itumike ili wale ambao wanafundisha shule za vijijini huku waume zao wakiwa mijini, waruhusiwe kuwafuata wenzi wao kwani ni utaratibu ndani ya jamii mke kumfuata mumewe, hivyo wasizuiwe," anasema.

Mweyekiti huyo anasema, anajua wapo walimu ambao hawataki maisha ya vijijini, lakini wengine wana sababu za msingi wakiwamo ambao wako kwenye ndoa na wenye matatizo ya afya na kwamba wasiwekewe marufuku.

ELIMU

NA REUBENI LUMBAGALA, DODOMA

# Mwongozo chakula na lishe shuleni, umma uelimishwe hasa umuhimu wake

Ni vigumu kwa binadamu kufanya shughuli zake kwa ufanisi akiwa na njaa au udhaifu mwilini unaotokana na kukosa lishe.

Halikadhalika, kwa wanafunzi shuleni, inawawia vigumu kujifunza kikamilifu ikiwa hawajala au hawapati chakula. Shughuli ya ujifunzaji kwa wanafunzi ni lazima iambatane na upatikanaji wa chakula ili waweze kujifunza vyema kwa ukamilifu.

Suala la wanafunzi kula chakula shuleni bado ni tatizo kitaifa iwe wa shule za msingi na sekondari changamoto hiyo hijapata jibu.

Ni shule chache zenye utaratibu wa kutoa chakula huku nyingi wanafunzi wakisoma bila chochote tumboni ikumbukwe, ukosefu wa chakula unaathiri ufanisi shuleni.

Mwanafunzi hawezi kuzingatia na kuelewa anachofundishwa na walimu wake kama anakabiliwa na njaa.

Hivyo basi, ni vyema suala la chakula na lishe shuleni likapewa msukumo na kipekee kama njia ya kuhamasisha mahudhurio mazuri kuwasadia wanafunzi kuelewa wanachojifunza na hatimaye kukuza ufaulu na taaluma kwa ujumla.



Watoto wa shule ya msingi wakifurahia kupata mlo shuleni. **PICHA: MTANDAO**

Oktoba 29, 2021, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilizindua Mwongozo wa Kitaifa wa Utoaji Huduma ya Chakula na Lishe kwa Wanafunzi wa Elimumsingi.

Madhumuni ya mwongozo huu ni kujenga uelewa wa pamoja wa wadau wa elimu na jamii ili kutekeleza kikamilifu mpango wa utoaji chakula na lishe kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari nchini.

Ni vyema jamii ikafahamu kuwa upatikanaji wa chakula na lishe shuleni ni jambo la msingi linalopaswa kutekelezwa bila upinzani kutoka kwa wazazi, walezi na wananchi.

Cha muhimu ni jamii ielimishwe namna chakula na lishe vilivyo vichocheo muhimu kuamsha na kuhamasisha wanafunzi kuhudhuria shuleni na kupenda kusoma.

Pasipo mahudhurio ya kuridhisha wanafunzi, hawawezi kupata ufanisi na tija ya ufundishaji na ujifunzaji haviwezi kuonekana.

Wazazi, walezi na umma uelimishwe uhusiano wa moja kwa moja uliopo kati ya upatikanaji wa chakula na mahudhurio bora ya wanafunzi ili jamii ihamasike kuchangia chakula kama vile mahindi, maharage, sukari, mafuta, mchele lakini kulima mboga, matunda, kufuga wanyama kama kuku na sungura ili wanafunzi wapate lishe bora shuleni. Wanafunzi wakihudhuria kikamilfu madarasani watajifunza kwa ukamilifu, na hivyo kufanya vizuri katika mitihani ya ndani na ya kitaifa.

Lishe bora inajenga afya na akili timamu, hivyo watoto wakipata chakula shuleni itasaidia katika kujenga afya bora na hivyo kumudu kuelewa yale wanayojifunza shuleni.

Suala la usomaji shuleni linahitaji wanafunzi kuwa na afya bora kwani usomaji ni kazi inayotumia ubongo na ili ubongo uweze kufanya kazi vizuri ni lazima mwanafunzi awe ameshiba.

Kwa hiyo, ni vyema jamii ikaeleweshewe kuhusu ushiriki wao katika kuwasaidia wanafunzi kupata chakula shuleni ili chakula hicho kiwasaidie wanafunzi kujifunza kwa urahisi.

Aidha, katika uzinduzi huo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Dk. Leornard Akwilapo, anasema:

"Natambua kwamba utoaji wa huduma ya chakula na lishe ni suala mtambuka, linalohitaji ushiriki wa sekta na wadau mbalimbali. Ni matumaini yangu kuwa kila mmoja atasoma mwongozo huu na kutekeleza majukumu yake ipasavyo."

Mwongozo wa chakula na lishe kwa wanafunzi uliotolewa na serikali ni dira katika kujenga uelewa wa jamii kuhusu umuhimu wa ushiriki wao katika kuhakikisha huduma ya chakula na lishe shuleni inatolewa na inakuwa endelevu kwa afya za wanafunzi na maendeleo ya taaluma. Vilevile, Dk. Akwilapo aliendelea kusisitiza:

> "Natambua kwamba utoaji wa huduma ya chakula na lishe ni suala mtambuka, linalohitaji ushiriki wa sekta na wadau mbalimbali. Ni matumaini yangu kuwa kila mmoja atasoma mwongozo huu na kutekeleza majukumu yake ipasavyo."

"Niwaombe wadau wetu wa maendeleo, mashirika yasiyo ya kiserikali, kampuni binafsi na vyombo vya habari kuendelea kushirikiana na serikali katika kuhamasisha ili kuhakikisha kuwa watoto wetu wanapata chakula wanapokuwa shuleni."

Ni vigumu serikali kufanikisha utekelezaji wa mwongozo huu kama wadau wengine hasa jamii hawatatoa ushirikiano, anaongeza.

Serikali imejitwika jukumu kubwa la kugharamia utekelezaji wa Sera ya Elimumsingi bila ada kuanzia shule za awali hadi kidato cha nne.

Pia serikali inagharamia uboreshaji na ujenzi wa miundombinu ya kutolea elimu kama vile madarasa, ofisi za walimu, vyoo vya wanafunzi na walimu, mabweni, mabwalo, nyumba za walimu na ununuzi wa vitabu vya kiada na ziada.

Hivi vyote vinagharimu fedha nyingi, lakini serikali inatimiza jukumu lake kwa kulitekeleza.

Jamii kwa upande wenu, jitahidini kushiriki kikamilifu katika kuchangia chakula ili wanafunzi ambao ni watoto wao wenyewe waweze kupata chakula wawapo shuleni.

Wizara ya Elimu ihakikishe shule zote za msingi na sekondari zinapata nakala za mwongozo wa chakula na lishe kwa wanafunzi ili uongozi wa shule zishirikishe bodi na kamati za shule kuhusu mwongozo huo.

Vilevile, viongozi wa serikali za mitaa kupitia mikutano yao na wananchi wawaelimishe kuhusu umuhimu wa kuchangia chakula na lishe ili wanafunzi wapate chakula wawapo shuleni.

Zama za wanafunzi kusoma wakiwa na njaa zimepitwa na wakati, jamii tusimame katika nafasi yetu kwa kuwawezesha wanafunzi kupata chakula na lishe bora shuleni.

Mwaka 2022 uwe wa utekelezaji wa mwongozo wa chakula na lishe kwa wanafunzi kwa mafanikio makubwa kwa shule zote nchini.

**Mwandishi ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko Kongwa Dodoma.**
**Maoni: 0620 800462.**



## Serikali yaridhia kuanza mgodi mpya dhahabu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imetoa ridhaa ya kutolewa kwa leseni za uanzishwaji wa mgodi mpya mkubwa wa dhahabu wa Nyanzanga utakaojengwa katika kijiji cha Sotta wilayani Sengerema mkoani Mwanza.

Mgodi mwingine ni wa uchimbaji madini ya Rare Earth Elements, utakaojengwa katika kijiji cha Ngwala mkoani Songwe.

Waziri wa Madini, Dotto Biteko, alibainisha hayo jijini Dodoma alipokuwa akitoa taarifa kuhusu maendeleo ya sekta ya madini kabla na baada ya uhuru.

"Vilevile, ikumbukwe kwamba, muda si mrefu mradi mkubwa wa uchimbaji wa madini ya Graphite utaanza mkoani Lindi huku tayari Kampuni ya Shanta Gold ikiendelea na ujenzi wa mgodi wa kati wa uchimbaji dhahabu wa Singida.

"Haya ni mapinduzi makubwa na mafanikio kwa serikali katika kipindi hiki cha miaka 60 ikizingatiwa na historia ya mahali tulipotoka," alisisitiza Biteko.

Alisema nchi inaendelea kufungua shughuli za uchimbaji na biashara ya madini kwani hadi kufikia Septemba 2021, leseni hai ambazo zimeshatolewa za utafutaji wa madini ni 1,044 , leseni 15 za uchimbaji mkubwa, leseni 161 za uchimbaji wa kati, leseni 34,000 za uchimbaji mdogo na leseni 1561 za biashara ya madini. Alisema kutolewa kwa leseni hizi kunamaanisha kuwa serikali inaweza kuongeza mapato zaidi kupitia sekta hiyo ya madini.

"Mfano halisi ni mwaka wa Fedha tulioumaliza mwezi Juni mwaka 2021 ambapo wizara ilikusanya Sh. bilioni 584.8 sawa na asilimia 111.03 ya lengo la kukusanya Sh. bilioni 524 ambazo wizara ilipangiwa na serikali izikusanye," alisema.

Kadhalika, alisema kutokana na kuanzishwa kwa masoko ya Madini, wizara kupitia Tume ya Madini imeendelea kufungua biashara ya madini kwa kuweka mazingira wezeshi na miundombinu rahisi ya kufanya biashara kwa uwazi na ufanisi.

Alisema tangu kuanzishwa kwa masoko hayo mwezi Machi, 2019, nchi ina jumla ya masoko ya madini 42 na vituo vya Ununuzi wa Madini 59 yaliyoenea katika mikoa mbalimbali.

Aidha, kupitia uwepo wa masoko hayo na vituo vya ununuzi, madini yenye thamani ya Sh. trilioni 3.19 yameuzwa na kuiwezesha serikali kukusanya Sh. bilioni 222.07 kama mrabaha na ada ya ukaguzi tangu kuanzishwa kwake.

"Ndugu wanahabari, haya ni mafanikio makubwa ikilinganishwa na tulipotoka. Ndugu wanahabari, uwepo wa masoko haya na namna yanavyofanya kazi umeifanya Tanzania kuwa mfano kwa nchi nyingi ambazo zimekuwa zikija na nyingine zikiendelea kuomba kujifunza namna serikali inavyosimamia masoko haya na sekta nzima kwa ujumla," alisema Biteko.

# Waziri: Marufuku uanzishaji holela masoko, minada ya mifugo na uvuvi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amepiga marufuku uanzishwaji holela wa masoko na minada ya mazao ya mifugo na uvuvi.

Aidha, amesema masoko hayo pamoja na minada hiyo ambayo imekuwa ikianzishwa katika maeneo mengi nchini inatumiwa na wafanyabiashara kukwepa kulipa kodi ya serikali.

Ndaki, aliyasema hayo juzi wakati wa kikao cha kupokea taarifa ya makusanyo ya maduhuli ya sekta ya uvuvi kutoka kwa maofisa wafawidhi wa vituo vya ulinzi wa rasilimali za uvuvi nchini kilichofanyika jijini Dodoma.

"Kiutaratibu ni lazima tukague na tusajili masoko na minada yote hapa nchini, lakini kuna watu wanajianzishia tu masoko kule halafu analiita soko lake la kimataifa, hapana hatuwezi kuendelea na hiyo habari ni lazima sheria na taratibu zifuatwe," alisema.

Ndaki, alimwelekeza katibu mkuu wa wizara hiyo anayesimamia Sekta ya Uvuvi, Dk. Rashid Tamatamah, kupitia upya masoko yote ya mazao ya uvuvi yaliyopo nchini na kujiridhisha kama yanastahili kusajiliwa na yale ambayo hayastahili yafutwe mara moja.

"Kinachosikitisha ni kwamba, huko wanakoanzisha haya masoko na minada hakuna wataalamu wetu hivyo kila mtu anaenda sokoni na kuchukua anachotaka bila kufuata utaratibu wowote ule, hatuwezi kuwa na serikali ya namna hiyo na Rais hatotuelewa ikiwa kila mahala tutakuwa na masoko na minada inayoendesha shughuli zake kiholela," alisisitiza.

Vilevile, alimwagiza Dk. Tamatamah kuwaandikia barua ya onyo maofisa wafawidhi wa vituo vyote vilivyokusanya maduhuli chini ya asilimia 50 ya lengo walilowekewa ambapo amesema kuwa hatua zaidi dhidi ya maofisa hao zitachukuliwa endapo hawatoongeza kiwango hicho.

"Ila huyu wa Mtera ambaye ameshindwa kukusanya hata shilingi, Katibu Mkuu naomba umwondoe kule na umpangie kazi nyingine kwa sababu ameshaonyesha wazi kuwa kazi hiyo ameshindwa," alisema Ndaki.

Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, alisisitiza kupitiwa upya kwa kanuni zinazoongoza biashara ya mazao ya uvuvi nchini ambapo alisema kuwa zilizopo haziendani na mahitaji ya soko kwa hivi sasa.

"Samaki wengi hawaingii viwandani kwa sababu ya mabadiliko ya kanuni tuliyoyafanya mwaka 2020 hivyo ninashauri tuboreshe kanuni hizo kwa sababu tumeshaona hasara kubwa tunayoipata na kama hivi viwanda vikifungwa kwetu itakuwa ni aibu na fedheha," alisisitiza Ulega.

Kadhalika, alimwomba Waziri Ndaki kuridhia mapitio ya kanuni hizo ili ziweze kufanyiwa mabadiliko huku akitolea mfano wa kanuni ya 'whole fish' ambayo alisema kuwa inapaswa kufanyiwa mabadiliko na kusimamiwa ipasavyo ili samaki aina ya sangara aweze kuchakatwa na hatimaye serikali kunufaika na tozo 13 zinazotokana na uchakataji huo.




Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Doroth Gwajima, akiwasilisha taarifa ya maendeleo ya wizara hiyo tangu Tanzania ilipopata uhuru mwaka 1961, kwenye ukumbi wa Habari Maelezo, jana jijini Dodoma, ikiwa ni mwendelezo wa maadhimisho ya miaka 60 ya uhuru huo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# UNDP yafarijika kushirikishwa vita ya rushwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MWAKILISHI Mkazi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Maendeleo (UNDP), Christine Musisi, ameeleza kufurahishwa kushirikishwa kwa shirika hilo katika vita dhidi ya rushwa nchini.

Alisema hayo jijini hapa wakati wa uzinduzi wa mradi wa matumizi ya teknolojia ili kupunguza vitendo vya rushwa katika sekta ya afya nchini.

Alisema shirika hilo limeanza na mradi kwenye sekta ya afya kutokana na ukubwa wake na kugusa maisha ya watu moja kwa moja. "Sekta hiyo ni kubwa, rushwa si inapoteza haki za msingi bali pia inapoteza maisha ya watu," alisema.

Alisema UNDP, itashirikiana na serikali kuhakikisha mradi huo unatekelezwa na inachukulia kama mradi wa mfano.

Alisema wataendelea kushirikiana na mashirika ya kimataifa likiwamo Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) na Shirika la Afya Duniani (WHO) kudhibiti na kupunguza rushwa nchini.

Kwa mujibu wa Musisi, ushirika huo upo katika mpango wake kupambana na rushwa katika jamii unaofadhiliwa na serikali za Norway na Sweden kupitia mshirika yao ya misaada ya Norad na SIDA ambapo jumla ya Dola za Marekani 300,000 zimetolewa.

Alisema gharama ya rushwa kwa jamii ni kubwa na kwamba katika mwaka 2017 taarifa ya Global Financial Integrity ilikadiriwa kwamba fedha zisizo halali (IFFs) kwa mwaka 2014 zilikuwa kati ya Dola za Marekani trilioni 1.4 hadi 2.5 .

Aidha, alisema Jukwaa la Uchumi Duniani linakadiria rushwa duniani ni zaidi ya asilimia tano ya pato la dunia (Dola trilioni 2.6).

Alisema anafurahi kuona mapambano dhidi ya rushwa kwa Tanzania ni ajenda ya kila siku.

Alisema ushiriki wa UNDP katika mradi wa kupambana na rushwa katika sekta ya afya umelenga kusaidia TAKUKURU kuwa na uwezo wa kukabiliana na changamoto hiyo kwa kuwa na uwezo wa kuchambua na kutathmini viashiria vya rushwa katika shughuli mbalimbali kwenye sekta hiyo.

Naibu Mkurugenzi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ( TAKUKURU), Neema Mwakalyelye, alisema mradi huo uliozinduliwa unalenga kuwezesha taasisi kuwa na uwezo wa kufanya uchambuzi kielektroniki kwa data zinazohusiana na utoaji wa huduma za afya nchini. Alisema serikali imeelekeza fedha na inataka kuwe na matokeo.

"TAKUKURU itahakikisha rushwa haipati nafasi, tunazuia rushwa zaidi kuliko kupambana, na serikali imewekeza kwa kiwango kikubwa kwenye teknolojia," alisema.

Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Grace Magembe, alisema mradi huo utamulika katika sekta ya afya kuhakikisha rasilimali zinazotolewa zinatumika kama ilivyokusudiwa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika lisilokuwa la Kiserikali la Sikika, Elinei Kiria, alisema hii ni hatua nzuri kuwezesha matumizi ya teknolojia katika kupambana na rushwa.





# Jiji Mbeya latajwa kinara wa rushwa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

HALMASHAURI ya Jiji la Mbeya, imetajwa kuwa kinara wa vitendo vya rushwa, huku Idara ya Ugavi na Manunuzi ya Jiji hilo ikiwa inaongoza.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Mkoa wa Mbeya, Denis Manumbu, akizungumza na wanahabari, alisema katika kipindi cha robo tatu ya mwaka kuanzia Julai hadi Septemba mwaka huu, Halmashauri ya Jiji la Mbeya inaongoza kwa vitendo vya rushwa.

Alisema TAKUKURU kipindi cha robo tatu ya mwaka imefanikiwa kufanya uchambuzi wa mifumo sita na kufuatilia utekelezaji wa miradi 16 ya maendeleo yenye thamani ya Sh. bilioni tano katika sekta ya afya, elimu, maji, barabara, madini na maendeleo ya jamii.

Miongoni mwa miradi iliyokaguliwa ni ujenzi wa Hospitali ya Igawilo wenye thamani ya Sh. bilioni 1.6, ujenzi wa barabara ya RRM Sh. milioni 531, ujenzi wa soko la madini Sh. milioni 245, jengo la mionzi Hospitali ya Wilaya ya Chunya Sh. milioni 150.

"TAKUKURU tumebaini vitendo vya rushwa katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya na idara inayoongoza kufanya vitendo hivyo ni Ugavi na Manunuzi. Vilevile taasisi binafsi nazo zimeongoza kwa vitendo hivyo kwa mujibu wa taratibu zetu," alisema na kuongeza:

"Tunaendelea kuchukua hatua mbalimbali kwa mujibu wa sheria zetu sambamba na kutoa elimu kwa lengo la kuondoa mianya ya rushwa."

Aliongeza kuwa katika kukabiliana na vitendo vya rushwa TAKUKURU inaendelea kutoa elimu kwa lengo la kuondoa mianya ya rushwa iliyopo na kuimarisha usimamizi wa miradi kwa kusisitiza uzingatiaji wa sheria na kanuni za manunuzi ya umma ili kupata miradi bora yenye kukidhi thamani ya fedha.

Katika kuhakikisha TAKUKURU inasogeza elimu ya kukabiliana na vitendo vya rushwa mkoani Mbeya, kipindi cha robo tatu ijayo kwa kushirikiana na vijana wa skauti watatoa elimu ya mapambano dhidi ya rushwa ikiwa na lengo la kujenga uadilifu, uwajibikaji na uzalendo kwa vijana walioko katika shule za msingi, sekondari, vyuo vya kati na vyuo vikuu.




Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera (kushoto), akiteta jambo na Mkurugenzi wa Mbolea ya Fertilux ya nchini Ufaransa, David Sebastian (kulia), baada ya kufungua mkutano mkuu wa mwaka wa wanahisa Tanganyika Farmers Association TFA, jijini Mbeya mwishoni mwa wiki. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

## Wawaomba wanawake kumpa sapoti Rais Samia

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WANAWAKE wamekumbushwa kuendelea kuunga mkono jitihada zinazofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan, katika kutekeleza miradi ya maendeleo ikiwamo inayolenga masuala ya kijinsia.

Rai hiyo imetolewa na Mkurugenzi wa Shule ya Paradise Mission Pre and Primary School, Ndele Mwaselela, wakati akizungumza na wanawake wajasiriamali wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya.

Amesema wanawake wa Mkoa wa Mbeya ni miongoni mwa waliojitokeza kuunga mkono jitihada za kuwaletea maendeleo wananchi kwa kuanzisha vikundi na shughuli mbalimbali za ujasiriamali ili kujiongezea kipato.

"Tuendelee kumwombea Rais Samia Suluhu Hassan afya njema ili aweze kutumiza azma yake ya kuwatumikia Watanzania, nawaomba wanawake mwendelee kuchapa kazi kwa bidii kuimarisha uchumi wa mtu mmoja mmoja," alisema Mwaselela.

Mwenyekiti wa kikundi cha wajane kilichopo Kata ya Uyole, Suzana Mchiwa, alisema wameamua kuanzisha kikundi hicho cha wajasiriamali ili kujitegemea kiuchumi kuliko kusubiri fedha za hisani au ndugu ambazo wakati mwingine za manyanyaso baada ya wenzi wao kufariki.

"Kikundi chetu kinajishughulisha na biashara mbalimbali kama vile kuuza maharage, kulima viazi, kusuka mikeka na shughuli zingine za kujiongezea kipato hitaji letu kwa sasa ni kupata mtaji ili kukuza mtaji," alisema Mchiwa.

Kwa upande wake mwanasheria wa kujitegemea wa Kampuni ya Aika Attorners, Aikande Lema, aliwapa ujasiri wanawake kupambana na kuacha woga katika kutafuta riziki.

# Watu 3,000 wapata chanjo ya corona MZRH

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

ZAIDI ya wananchi 3,000 wamepata chanjo ya ugonjwa wa Uviko-19 katika Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya (MZRH), huku ikieleza kuwa idadi hiyo inatokana na juhudi za wataalamu wa sekta ya afya kuendelea kutoa elimu juu ya umuhimu wa chanjo hiyo.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa MZRH, Dk. Godlove Mbwanji, idadi ya watu kuchanja inaongezeka kila siku na kwamba wanaendelea kutoa elimu ya hamasa ili watu wachanjwe.

"Tunayo furaha kwamba zoezi la chanjo ya Uviko-19 linaendelea kufanyika vizuri katika vituo vyetu viwili ambavyo ni Hospitali ya Wazazi Meta na Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya, tulianza na chanjo ya Johnson and Johnson na hii mpya ya Sinopharm na kufanikiwa kuchanja watu 3054," alisema Dk. Mbwanji.

Alifafanua kuwa jumla ya watu 77 wamepata chanjo mpya Sinopharm kutoka nchini China na zoezi linaendelea vizuri tunaimani idadi ya watu itaongezeka huku watu 2,977 wakipata ya Johnson and Johnson. Katika hatua nyingine, Dk. Mbwanji alisema kasi ya magonjwa yasiyoambukizwa inaongezeka nchini, aliwaomba Watanzania kuendelea kuzingatia mlo kamili na kufanya mazoezi.

Alisema wakati tunaadhimisha wiki ya magonjwa yasiyoambukizwa duniani ni vyema watu wakajitokeza kupima afya zao na kupewa ushauri na namna ya kujikinga.

Mmoja wa madaktari katika Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya, Joyce Komba, aliwahamasisha wananchi kufika katika hospitali hiyo kupima magonjwa mbalimbali yasiyoambukizwa kwa maelezo kuwa kuna vifaa vya kisasa na wataalamu wa kutosha kutoa huduma hizo.

Mkazi wa Jiji la Mbeya, Theodory Mhanga, alisema tangu achanjwe hakuna madhara yoyote ya kiafya aliyoyapata na anaendelea vyema na shughuli zake za uzalishaji.



## Wanaopinga uwekezaji Anglikana waonywa

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

WAUMINI wa Anglikana Zanzibar wametakiwa kudumisha amani na kuwa watulivu, huku uongozi ukitafuta wawekezaji kwa ajili ya kuwekeza na kuitumia rasilimali ya ardhi kulinufaisha kanisa kuingiza mapato na kujiendesha.

Akizungumza jana na waandishi wa habari huko Kiungani Unguja, Askofu wa Anglikana Zanzibar, Dk. Michael Hafidh, alisema kanisa limejipanga zaidi katika uwekezaji kufuatia sera ya Serikali Zanzibar kujikita katika uwekezaji kwa kutumia rasilimali zilizopo ikiwamo ardhi.

Alisema wapo wawekezaji waliojitokeza na kuonyesha nia ya kuwekeza katika miradi ya uwekezaji ambapo uongozi wa kanisa unafanya utafiti zaidi kwa kupitia majina ya wawekezaji hao kwa ajili ya watakaokidhi vigezo.

"Mikakati ya uongozi wa kanisa la Anglikana Zanzibar ni kufunguwa milango ya fursa za uwekezaji kwa wawekezaji mbalimbali wenye nia ya kuwekeza kwa kutumia vitega uchumi vyetu vilivyopo ambavyo ni ardhi...wapo wawekezaji wameonyesha nia na tupo tunapitia majina hayo," alisema.

Hata hivyo, Askofu Hafidh alikemea vikali baadhi ya tabia ya waumini wa kanisa hilo kuendekeza migogoro na mivutano pamoja na chuki na uhasama, ambavyo vinaweza kurudisha nyuma juhudi zao za uwekezaji pamoja na kulivunjia hadhi na heshima kanisa hilo.

Alieleza kuwa baadhi ya waumini wa kanisa hilo wanapinga juhudi za uwekezaji katika kanisa kwa kutumia rasilimali za ardhi. Akifafanua zaidi, alisema baadhi ya viongozi wa kanisa hilo wameweka mbele maslahi binafsi na kuona miradi inayotekeleza inakuwa sehemu ya miradi yao, kitendo ambacho alisema hakikubaliki katika kuendesha taasisi hiyo.

Aidha, alisema wapo baadhi ya viongozi na waumini wamekuwa wakipinga juhudi za kanisa katika uwekezaji katika eneo la Kiungani karibu na Bahari ya Hindi huko Kilimani Unguja, huku wakitaka kuona kwamba maslahi yao binafsi yanapatikana.

"Hatuwezi kufikia maendeleo ya kweli katika kuimarisha kanisa kama watakuwapo baadhi ya viongozi wakiendesha malumbano na migogoro, huku wakipinga juhudi zinazochukuliwa na kanisa katika uwekezaji," amesema.

# Othman Masoud ataka ujenzi mfumo sahihi wa utawala

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema kazi kubwa ya serikali ni kujenga mfumo sahihi wa utawala wenye uwezo wa kutengeneza fursa kwa watu wote.

Pia kuwawezesha wananchi kuzitumia kwa maslahi yao na taifa kwa jumla.

Othman aliyasema hayo juzi alipozungumza katika kungamano maalum la kumuenzi aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Hayati Maalim Seif Sharif Hamad mjini Zanzibar.

Aidha, alisema pia ni muhimu kuwapo mfumo bora utakaosaidia kuwawezesha wananchi kuzitumia fursa za kiuchumi zilizoandaliwa kwa kuwekeza katika kutengeneza sera bora na usimamizi wake na kuiwezesha serikali kuwa na uwezo wa kutoa huduma za kiuchumi na kuharakisha maendeleo ya taifa.

Alisema hatua hiyo itawezesha wananchi kujiajiri na kuajiriwa sambamba kuimarisha na kuwapo nyenzo muhimu za kufikia jitihada za pamoja za maendeleo.

Alisema kuna haja kubwa sasa Zanzibar kuangalia kwa tathmini ya ukubwa wa serikali na kufanya mageuzi makubwa ya shughuli zinazofanywa kuanzia ngazi ya serikali za mitaa ambapo kunahitajika kuimarishwa kwa kuwa zipo kikatiba.

Alisema hatua hiyo itasaidia wananchi kurejesha imani kwa serikali yao na kuondosha uhasama na mifarakano inayotokana na sababu za kisiasa, hivyo kuendeleza maridhiano ya kweli ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa Zanzibar.

Alibainisha kwamba haitowezekana kujenga umoja wa kitaifa na maridhiano ya kweli kama hakujarejeshwa imani ya watu juu ya ushiriki wao katika kuendesha nchi yao kupitia majukwaa ya siasa na uchaguzi katika ngazi mbalimbali.

Alisema ni lazima kuhakikisha kwamba siasa ni jukwaa sahihi la wananchi katika kuamua hatima ya nchi yao kwa kupitia uwanja wa siasa.

Alisema ni muhimu kurejea imani na kuimarisha kuaminiana kati ya viongozi wa kisiasa na wafuasi wao ili wananchi kufahamiana na kuaminia kwa kuwa wakweli.

Alisema mazingira yanavyojionyesha katika serikali ya umoja wa kitaifa hivi sasa ni kuwapo kwa nia njema na utayari wa viongozi, jambo ambalo litawezesha kuimarika na kuendelea kujenga umoja miongoni mwa wananchi.

Akizungumza katika kongamano hilo kuhusu uzoefu wake wa kumtambua Maalim Seif, Rais Msaafu wa awamu ya sita Dk. Amani Abeid Karume, alisema anamtambua kama ni mtu mstahimilivu na mvumilivu aliyeweka mbele maslahi na maendeleo ya wananchi wakati wote.

Alisema licha ya kuwepo misukosuko kadhaa ya kisiasa katika kipindi kirefu, lakini Maalim Seif hakukata tamaa na wakati wote alipenda kutatua migogoro kwa njia ya majadiliano ambayo ndio jukwaa sahihi la kuleta umoja na maridhiano.

Mjane wa Maalim Seif, Mama Awena Sinan Masoud, alisema siri kumbwa ya Maalim Seif ni kutokata tamaa, kuweka mbele dini na dunia katika kuwatumikia wananchi.

Alisema Maalim Seif alitenga vyema muda wake katika kufuatilia miongozo muhimu ya quraan, jambo lililomsaidia sana katika kuwa mtu anayesamehe na mvumilivu katika masuala na changamoto mbalimbali za kisiasa na kijamii alizokumbana nazo.



Makamu wa kwanza wa Rais, Othman Masoud (kushoto), akizungumza na baadhi ya viongozi akiwamo Rais mstaafu Amani Karume (kulia), Ismail Jussa Ladhu (wapili kulia), Jaji Warioba (watatu kushoto) na Muhamed Zara (wapili kushoto) baada ya kumalizika kwa kongamano la kumuezi Maalim Seif Sharif Hamad mwishoni mwa wiki Mjini Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Waziri: Vijana lindeni amani, utulivu kuvutia wawekezaji

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Kilimo, Maliasili, Umwagiliaji na Mifugo, Soud Nahoda Hassan, amewataka vijana kulinda amani na utulivu uliopo nchini ili kuwavutia wawekezaji kuwekeza katika sekta mbalimbali kwa lengo la kukuza uchumi wa taifa.

Aliyasema hayo jana ofisi za Baraza la Mji Kati Mkoa wa Kusini Unguja, wakati akifungua mafunzo ya kilimo cha mapensheni kwa umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Kati.

Alisema kutokana na umoja na mshikamano uliopo Zanzibar, wawekezaji wengi wamejitokeza kuekeza katika sehemu tofauti.

Alisema serikali ya awamu ya nane inayoongozwa na Dk. Hussein Ali Mwinyi imetenga fedha kwa ajili ya vijana kujiajiri katika sekta ya kilimo na ufugaji kwa lengo la kuwasaidia vijana kuondokana na changamoto ya kusubiria ajira kutoka serikalini.

Aidha, aliwataka vijana kuyatumia mafunzo watakayopatiwa kujiendeleza katika kilimo na kuchangamkia fursa za mikopo itakayotolewa na serikali na taasisi mbalimbali za fedha.

Pia, aliwaahidi vijana hao kuwatafutia wafadhili kutoka ndani na nje ya nchi watakaowekeza katika sekta ya kilimo na ufugaji sambamba na kuwatafutia soko la uhakika kwa bidhaa watakazozalisha.

Akizungumzia suala la ajira, alisema kuwa bado ni changamoto kwa ajira za serikali, hivyo aliwataka vijana kubuni miradi mbalimbali itakayowapa ajira kwa kujiingigizia kipato cha uhakika na kujikwamua kiuchumi.

Naye Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Vijana, Shaibu Ibrahim Mohammed, alisema kupitia idara hiyo itahakikisha itawasimamia vijana katika miradi watakayoianzisha ili kuona inakuwa endelevu na kuwasaidia kufikia malengo yao.

Mwenyekiti wa umoja huo wa vijana, Fidenis Danien, alisema bado ushirika wao unakabiliwa na ukosefu wa vitendea kazi kwa ajili ya kilimo na mifugo ikiwamo kukosekana ushirikiano kati yao na baadhi ya viongozi.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

GARI INAUZWA AINA YA VOLKSWAGEN TOUREG YA MWAKA 2004 NAMBA DDV RANGI NYEUSI. INATEMBEA NA IKO KWENYE HALI NZURI SANA. BEI NI TSH. 15,000,000/- PIGA SIMU NAMBA 0762 810 451.

## OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

## KUPOTEA KWA CHETI



**PATRIC JOHN MARTINS** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S4202/0034** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary **FRANCIS MARIA LIBERMANN** mwaka 2018,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa AR/SH.25/JANG/VOL11/68

## KUPOTEA KWA CHETI/RESULT SLIP



**JOSHUA MUSA BASU** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S2624/0084 kilichotolewa na Baraza la Mitihani kupitia **NAMONGE SEKONDARI** mwaka 2018. Result Slip ya kidato cha sita yenye index namba **S0706/0512** iliyotolewa na **KALANGALALA SEKONDARI mwaka 2021. Yeyote** atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi.Taarifa ya polisi: DAR/MSI/RB/524452/2021.

## KUPOTEA KWA CHETI



**YASINI SHABANI SINTOO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **P0334/0075** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule/kituo MWENGE SECONDARY mwaka 2018, yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **SIN/SIN/RB/5254/2021**

## KUPOTEA KWA CHETI



**GIFT WILLIAM ABRAHAM** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.1150/0051** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia MUUNGANO SEKONDARI mwaka 2016. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.Taarifa ya Polisi: **DAR/KIG/RB/36054/2021.**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI
IDARA YA UHAMIAJI

## OMBI LA URAIA



SAMI ALI TAHER RAIA WA LEBANON AMBAYE PICHA YAKE IMEONESHWA HAPO JUU, MWENYE PASSPORT NAMBA RL.LR1755132

ANAOMBA URAI JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KWA MHESHIMIWA WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI, AMEISHI NCHINI TANGU MWAKA 1998 KATIKA MKOA WA MWANZA AKIJISHUGULISHA NA BIASHARA.

MTU YEYOTE MWENYE SABABU YA KUPIGA MWOMBAJI ASIPEWE URAIA, ATUME TAARIFA YAKE YA MAANDISHI ILIYOSAINIWA KWA KAMISHINA JENERALI WA UHAMIAJI S.L.P.DAR ES SALAAM KWA KUTUMIA KUMB NA. AC :27/340/5325 "F"

..............................................................................

K.n.y. KAMISHINA JENERALI WA UHAMIAJI

## KUBADILISHA JINA



Mimi **JULIANA NDUNGE JACKSON** nikiwa na akili zangu timamu nimeamua kubadilisha jina langu kutoka **JULIANA NDUMGE MTENGA** na kuwa **JULIANA NDUNGE JACKSON** kuanzia leo 5/11/2021 Taratibu zote za kisheria zimefuatwa

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**LULU BAHATI FULGENCE** anatangaza kupotelewa na result slip ya kidato cha nne yenye **index namba S.3648/0028** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary THE OFLOW NGOWI MEMORIAL mwaka 2020, yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi.Polisi taarifa **DAR/CHA/RB/509502/2021**

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**NASRI SALUM MAULIDI** anatangaza kupotelewa na Result Slip ya kidato cha nne yenye index namba S.0812/0097 iliyotolewa na MAHIWA SEKONDARI mwaka 2020. Pamoja na Living Certificate na cheti cha kuzaliwa.Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/MBA/RB/489078/2021.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

MARIAMU MWIDUCHI OMARI ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI T 528 CVC AINA YA TOYOTA CARINA KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI TAARIFA YA POLISI KAH/ RB/528/2021

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA
AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.86 OF 2021**

**In the matter of the Estate of the MUSSA ABINEL DANIEL of Mkalama within City Council of Dodoma**

**And**

**In the matter of an application for letters of Administration by OLIVIA LABANI MSONGA.**

**GENERAL CITATION**

**(RULE 75 OF PROBATE RULES GN 369 OF 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioners.

Objections to the grant should be filed on or before 25 Day of November 2021.

**Dated at Dodoma this 08 day of November, 2021**

Dated at Dodoma this 08 Day of November 2021.

PETITIONER

Presented for filing this 08 day of November, 2021

RESIDENT MAGISTRATE

RESIDENT MAGISTRATE DODOMA DISTRICT

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA
AT DODOMA
PROBATE AND ADMINISTRATION
CAUSE NO.171 OF 2021
In the matter of the Estate of the late
HUDSON YOHANA MADINDA
Of Mpamaa within Dodoma City
And
In the matter of application for letters of Administration by GRACE HUDSON MADINDA**

**GENERAL CITATION
(Rule 75 of Probate Rules Gn.369 of 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 29 day of November,2021.

Dated at Dodoma this **8TH day of November, 2021.**

RESIDENT MAGISTRATE

RESIDENT MAGISTRATE DODOMA DISTRICT

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA
AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.153 OF 2021**

**In the matter of the Estate of the late ALOYCE YAMBAZI TWIGA Of Mbwanga within Dodoma City**

**And**

**In the matter of application for letters of Administration by CHRISTINA ALOYCE YAMBAZI**

**GENERAL CITATION**

**(Rule 75 of Probate Rules Gn.369 of 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 15/11/2021.
Dated at Dodoma this 27 day of October, 2021.

COURT SEAL

.....................................
RESIDENT MAGISTRATE

RESIDENT MAGISTRATE DODOMA DISTRIC

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Njombe**

**Kituo cha Njombe Mjini
Mkoa Njombe**

**Usimamizi wa Mirathi Na. 65/2016.**

**Ezekiel Petro Kihaka..............................Marehemu**

**Franka Nziku.......................................Msimamizi**

**TAARIFA KWA UMMA**

**MAOMBI YA KUTANGAZA KUFUNGA MIRATHI**

Kwa wote wanaodai kuwa na haki na marehemu aliyotajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia orodha ya mali za marehemu na hesabu za mirathi katika jalada la mirathi. Mapingamizi yoyote kuhusu orodha ya mali na au hesabu za mirathi hii yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya siku ya tarehe 18th ya Mwezi wa Desemba Mwaka 2021.
Imetolewa na Hakimu mkazi leo siku ya tarehe 05th Octoba, Mwaka 2021.

HAKIMU MKAZI

HAKIMU MKAZI NJOMBE - MJINI

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya MOROGORO**

**Kituo Cha URBAN Mkoa.... Morogoro**

**Usimamizi wa Mirathi Na 321/2021**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU HAMISI JUMANNE MALINDA WA MOROGORO
KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA CHIKU HAMISI MALINDA**

**TANGAZO**

**(Kanuni ya 5 (2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo tarehe 7 Mwezi 12 Mwaka 2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo .
**Zingatia**
Endapo Kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa

- Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani na waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia * Futa isiyohusika

Imetolewa Leo Tarehe 4 Mwezi 11 Mwaka 2021

HAKIMU

HAKIMU MAHAKAMA YA MWANZO MJINI MOROGORO

**FORM 78 APPOINTMENT OF ADMINISTRATOR OF SMALL ESTATE
(Section 76, Rule 93)
IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF (MISUNGWI) DISTRICT
AT MISUNGWI
PROBATE AND ADMNISTRATION
CAUSE NO. 01 OF 2021**

In the Matter of the Estate of the late WILBARD RWEYEMAMU
And
In the Matter of Application for LETTERS OF ADMINISTRATION By FAUSTER RWEYEMAMU BE IT KNOWN that FAUSTER RWEYEMAMU of P.O.BOX 194 TABORA is hereby appointed Administrator of the estate of the Late WILBARD RWEYEMAMU (deceased), who died at BUGANDO REFERRAL HOSPITAL on the 31st day of March 2006 the said FAUSTER RWEYEMAMU having undertaken well and faithfully to administer the said estate.
Given under my hand and the seal of the Court this 14th day of September 2021.

Resident Magistrate

RESIDENT MAGISTRATE MISUNGWI

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**AHAMED JIMMY HASSAN** Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T. 116 BPL,** aina ya **NOAH.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake, Taarifa ya jeshi la polisi, **KAH/RB/TR/559/2021.**

**OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KITAIFA

# WB yatoa mkopo wa mabilioni mradi wa Tanzania ya kidijitali

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

BENKI ya Dunia (WB) imetoa mkopo wa Dola za Kimarekani milioni 150, kwa ajili ya kutekeleza mradi wa Tanzania ya kidijitali wa miaka mitano ambao utajihusisha na kuboresha miundombinu ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhandisi Andrea Kundo, alibainisha hayo jana jijini hapa wakati alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari baada ya kutembelewa na ujumbe kutoka Benki ya Dunia.

Alisema moja katika ya malengo ya mradi huo ni kuhakikisha kuwa miundombinu ya TEHAMA inafanyiwa maboresho makubwa ili kurahisisha utoaji wa huduma za kidijitali.

"Maboresho katika miundombinu ya TEHAMA ni sawa na kufanya maboresho katika barabara kama itakuwa na lami basi gari linaweza kupita vizuri hivyo hivyo katika miundombinu ya TEHAMA lazima kuwepo na maboreshaji ili kuweza huduma hii kufikia wananchi kwa uhakikika na gharama nafuu," alisema Kundo.

Alisema, moja kati ya vikwazo hivi sasa ni huduma duni za Teknolojia ya Habari na Mawasilino lakini kupitia mradi huo changamoto zote zinakwenda kufanyiwa kazi.

"Unakuta wakati mwingine mtu unatuma fedha, lakini unachelewa kupata ujumbe wa kukujulisha, hii ni kutokana na huduma duni za TEHAMA hivyo mradi huu unakwenda kujibu maswali yote na kuondoa kero zilizopo," alisisitiza.

Alisema, mradi huo wa Tanzania ya kidijitali unalenga kukuza maendeleo ya kidijitali kama kichocheo kikuu cha ukuaji wa viwanda, utengenezaji wa ajira, utaoji wa huduma na ufanisi wa serikali.

"Mpango wa FYDP 111 unaweka lengo la kuhakikisha kuwa mtandao wa kasi unafikia asilimia 80 ya wananchi ifikapo mwaka 2025, pamoja na huduma za mtandao wa intaneti kwa wote," alisisitiza.

Alisema lengo ni kuinua mchango wa sekta ya mawasiliano uliokadiriwa kati ya asilimia mbili hadi tatu na zaidi ya pato la taifa ifikapo mwaka 2025.

"Tunaishukuru serikali ya awamu ya sita kwa kutusaidia kupata mkopo huu kutoka Benki ya Dunia tunajipanga vizuri kuhakikisha kuwa mradi huu unakamilika na kuweza kusaidia Watanzania kupata huduma bora na kwa gharama nafuu," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao, Benedct Ndomba, alisema mradi huo ukiimalika utawezesha huduma ya serikali mtandao isiishie mikoani pekee bali iwafikie hadi wananchi wa ngazi ya chini.

"Mradi huu utawezesha wananchi kupata huduma bora na kwa gharama nafuu, tupo tayari kutoa ushirikano wetu pamoja na utaalamu wetu ili kufanikisha mradi huu," alibainisha Ndomba.

Kiongozi wa msafara wa ujumbe huo kutoka Benki ya Dunia, Dk. Tim Kelly, alisema lengo la ziara hiyo ni kuja kuona ni kwa namna gani Tanzania ipo tayari kwa ajili ya kutekeleza mradi huo wa miaka mitano.

# H/shauri 55 zakopeshwa bil. 50/- upimaji ardhi

**Na Ibrahim Joseph, DODOMA**

SERIKALI imetoa mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 50 kwa halmashauri 55 nchini kwa lengo la kusaidia miradi ya upimaji ardhi na uendelezaji miji kwenye maeneo yao.

Aidha, halmashauri zilizopokea mikopo hiyo zimetakiwa kuhakikisha zinatumika vizuri kwa malengo yaliyokusudiwa na kuzirudisha kwa wakati, ili halmashauri zingine zipate fursa za kukopa.

Waziri wa Fedha na Mipango, Mwigulu Nchemba, alisema hayo wakati wa hafla ya utiaji saini wa makubaliano ya utoaji wa fedha za mikopo ya utekelezaji wa programu ya kupanga ,kupima na kumilikisha ardhi nchini, iliyofanyika jana jijini hapa.

Nchemba, alisema serikali imetoa kiasi cha Sh. bilioni 50 kwa halmashauri 55 nchini kupitia wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ili kusaidia upimaji wa ardhi kwenye maeneo yao.

Alisema lengo la serikali kutoa mikopo hiyo ni kuziwezesha halmashauri hizo kupima ardhi na kuondoa ujenzi holela kwenye maeneo hayo.

Alibanisha kuwa serikali itaendelea kutoa fedha hizo, kutokana na hali ya bajeti itakavyokuwa imepangwa hivyo waliopata mikopo hiyo wanatakiwa kuonyesha mifano kwa wengine watakaohitaji.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) Ummy Mwalimu, aliishukuru serikali kwa mkopo huo, ambao utakuwa chachu ya maendeleao kwenye halmashauri mbalimbali nchini.

Mwalimu, alisema kupatikana kwa fedha hizo imeongeza vipaumbele alivyokusudia kwenye utendaji wake wa kazi alivyojiwekea wakati anaingia kwenye wizara hiyo.

Alivitaja vipaumbele hivyo kuwa ni huduma za afya ,elimu msingi,kuwawezesha wananchi kiuchumi hasa akinamama walemavu na vijana,ujenzi wa miundombinu ya barabara.

Waziri huyo, alisema kwa sasa ameongeza kipaumbele cha tano ambacho ni upimaji wa ardhi kwenye halmashauri mbalimbali nchini.

Alisema kuwa upatikanaji wa fedha hizo zitaenda kuchochea ukuaji wa uchumi kwa wanachi pamoja na halmashauri husika.

Kwa upande wake Waziri wa Ardhi,Nyumba na Maendeo ya Makazi ,William Lukuvi alisema fedha hizo zitakomesha ujenzi wa nyumba holela kwenye miji.

Lukuvi alisema siku za nyuma halmashauri zilikuwa zikiomba mikopo kutoka taasisi za kifedha, lakini awamu hii serikali imechukua jukumu hilo.

Aidha alisema mikopo hiyo imetolewa na serikali kutokana na andiko lililoandikwa na halmashauri husika kuhusu kazi za fedha hizo.

Alibanisha kuwa jumla ya halmashauri 78 ziliomba mikopo hiyo, lakini waliofanikiwa ni halmashauri hizo 55 na watakuwa wakitoa mikopo hiyo kutokana na bajeti.


EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

**OMBI LA KUONESHA NIA KWA AJILI YA UTOAJI WA HUDUMA YA SAMANI ZA OFISI PAMOJA NA UWEKAJI WA SAMANI KATIKA OFISI**
**KUMBUKUMBU 0010007217**

Kampuni ya Kimataifa ya Mafuta na Gesi ya TotalEnergies East Africa Midstream B.V. inaalika taasisi zenye weledi na uzoefu kuonesha nia ya kutoa huduma ya uwekezaji wa vyombo vya ofisini.

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litakalofukiwa chini ya ardhi litakalovuka mipaka ya nchi mbili na litakalosafirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha mafuta hayo kwenda katika masoko ya Kimataifa. Bomba hili litaanzia Kabaale katika wilaya ya Hoima nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoani Tanga nchini Tanzania. Urefu wa Bomba ni kilomita 1,443, kati ya hizo, kilomita 1,147 zitakuwa Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI KUHUSU MAWANDA YA HUDUMA:**

- EACOP inahitaji huduma kutoka kwa mtoa huduma mwenye uzoefu na sifa nzuri ya kutoa huduma za samani za ofisi pamoja na kuziweka katika ofisi ipasavyo.
- Madawati na meza za kufanyia kazi (vituo vya kazi vinavyoweza kuongezwa na kupunguzwa urefu wakati wa matumizi).
- Meza na viti vya vyumba vya mikutano (kiwango cha kawaida na kiwango cha vyumba vya mikutano).
- Viti vya ofisini vinavyoweza kurefushwa au kufupishwa na vilivyo undwa kwa ajili ya kutoa usaidizi bora kwa mgongo wakati wa kukaa (ergonomic).
- Makabati ya kuhifadhi mafaili (Credenzes).
- Kabati za kuhifadhi vitu mbali mbali.

**VIGEZO MUHIMU:**

Taasisi zitakazoonesha nia zinaalikwa kuambatanisha maombi yao pamoja na taarifa zifuatazo:

- Uthibitisho wa Uzoefu, utendaji, na uwezo katika kutekeleza kazi zilizoainishwa katika mawanda ya kazi, kwa viwango vya juu nchini Tanzania, kwa kufuata viwango vya kitaifa na kimataifa (ikiwa ni pamoja na Viwango vya Shirika la Fedha la Kimataifa (IFC), na uzoefu wa angalau miaka 5 katika utendaji wa huduma kama hizo ndani ya Tanzania au Kimataifa.
- Uthibitisho wa watendakazi husika wenye vigezo na uzoefu katika uwekaji wa samani katika ofisi.
- Inashauriwa, mwonyesha nia atume maombi ya kusajiliwa na kanzi data ya EWURA (LSSP) kama mtoaji namsambazaji wa huduma ndani ya nchi wakati wa kuwasilisha ombi la kuonesha nia ya kutekeleza shughuli za progamu.
- Kuzingatia Kanuni za maudhui ya Ndani za mwaka 2017 pamoja na tafsiri ya Kampuni ya Ndani.
- Uwezo wa kifedha kuweza kutoa huduma zinazohitajika ikiwa ni pamoja na kuwasilisha mahesabu ya fedha ya mwaka 2017.

- Uthibitisho wa sera ya ndani ya Afya, Mazingira na Usalama, taratibu na mchakato kulingana na viwango vya ndani vya viwanda vya kazi husika.
- Uthibitisho wa usajili katika mamlaka husika ndani ya nchi kwa ajili ya utoaji wa huduma husika.
- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na cheti cha uthibitisho wa kulipa kodi kwa mwaka wa fedha uliopita.

Taasisi zenye nia ya kuleta maombi na ambazo zina uwezo na rasilimali za kutekeleza shughuli au kazi zilizoorodheshwa hapo juu zinapaswa kueleza nia yao kwa lugha ya kiingereza pamoja na kuambatanisha nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe kwa **eacoptz.eoi.1000001@totalenergies.com** (ukubwa wa barua pepe 20 Mb) saa au kabla ya saa **11 jinni** za Afrika Mashariki (EAT) tarehe **....Novemba 2021.** Kichwa cha Habari cha barua pepe kiwe ni kumbukumbu namba husika tu. Kichwa cha Barua Pepe kiwe ni **0010007217.**

**Muhimu:** Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na taasisi zitakazoonyesha nia iii kutengeneza orodha ya taasisi za awali zenye vigezo vinavyotakiwa. Taasisi zitakazokidhi vigezo iu ndiyo zitapokea na kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA) pamoja na mwaliko wa kuwasilisha zabuni katika kuendeleza mchakato wa zabuni. Maelezo yote ya kuonyesha nia yanapaswa kuandikwa kwa lugha ya Kiingereza.

216552602

# MALINDI KILELENI LIGI KUU Z'BAR, YAIPANIA ZIMAMOTO

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya Malindi imekaa kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar baada ya kufikisha alama saba sawa na KMKM FC, ambayo inazidiwa kwa tofauti ya mabao ya kufunga wakati huu timu zote zikiwa zimeshuka dimbani mara tatu msimu huu.

Kama ilivyo kwa KMKM, Malindi nayo imeshinda michezo miwili na sare moja huku ikiwa haijaruhusu nyavu zake kutikiswa na imecheka na nyavu mara tatu tofauti na wapinzani wao hao ambao wana mabao manne yakufunga na mawili ya kufungwa.

Malindi ilipanda kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo juzi baada ya kutoka sare tasa na Polisi katika mechi iliyopigwa Uwanja wa Gombani Kisiwani Pemba.

Akizungumza na gazeti hili Kocha wa Timu ya Malindi, Abdulghani Himid Msoma, alisema katika mechi tatu walizocheza licha ya kupata mafanikio, lakini bado kikosi chake hakijapata muunganiko unaotakiwa kati ya wachezaji wapya na wa zamani.

Alisema pia baadhi ya wachezaji wanashindwa kuwa wabunifu au kutumia mbinu za kiuchezaji hususan wanapokuwa katika lango la wapinzani.

Aidha, alisema katika mchezo wao wa raundi ya nne ambao watakutana na Zimamoto, amejipanga kuhakikisha wanashinda kwa kuwa mechi hiyo ndiyo anatarajia imwonyeshe mwanga wa wachezaji wake.

Alisema anaiheshimu timu ya Zimamoto kwa kuwa ni timu kubwa na inauzoefu mkubwa katika Ligi Kuu Zanzibar, hivyo lazima wachezaji wake wacheze kwa umakini mkubwa ili lengo la ushindi litimie.

Katika msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 16, nafasi ya tatu inashikwa na JKU yenye alama sita sawa na Black Sailor iliyopo nafasi ya nne kutokana na kuzidiwa kwa tofauti ya mabao ya kufunga na kufungwa huku Zimamoto ikifuata kwa alama zake tano.

**TUKUTANE Z'BAR...**




Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi (katikati), akiwa na washambuliaji wake, Heritier Makambo (kushoto) na Fiston Mayele, timu hiyo inatarajia kuelekea Zanzibar leo kucheza mechi mbili za kirafiki dhidi ya Mlandenge na KMKM. **PICHA: MAKTABA**

# Viongozi Ligi Kuu someni kanuni - TPLB

**Na Adam Fungamwango**

BODI ya Ligi nchini (TPLB), imesema imebaini kuwa viongozi wengi wa klabu nchini hawasomi au kuzipitia kanuni, hivyo kuwasababishia wao na klabu zao kupata matatizo mengi ya kufungiwa au kulipishwa faini.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa TPLB, Almasi Kasongo, alisema hayo jana wakati akitoa ufafanuzi wa adhabu mbalimbali zilizotolewa na Kamati ya Utendaji na Usimamizi wa Ligi ya Bodi ya Ligi Kuu Tanzania Bara kilichokaa Novemba 5, mwaka huu.

Pamoja na mambo mengine, Kasongo alieleza juu ya tabia ya timu kugomea kuingia kwenye vyumba vya kuvalia ambayo kwa sasa imeanza kuwa sugu.

"Utaratibu wa timu kugomea kuingia kwenye vyumba vya kuvalia ni kosa kikanuni, lakini inawezekana ikawa siyo kosa pale utaratibu utakapozingatiwa kwa viongozi, kocha au wachezaji ambao wanaona kuna kitu hakipo sawa kwenye vyumba, wanapaswa kumshirikisha kamisaa wa mchezo, daktari au mratibu," alisema Kasongo.

Alisema baada ya watu hao kuvikagua na kujidhihirisha, kamisaa ataandika taarifa yake na kamati ikiona kama kuna sababu za msingi, basi klabu iliyofanya hivyo haitoadhibiwa.

"Bahati nzuri tuna kanuni rafiki, ambazo lengo ni kwamba michezo yetu pia iwe rafiki, lakini viongozi wengi hawasomi kanuni, au hawazipitii na kama wanafanya hivyo basi wanakwenda kwenye mechi wakiwa tayari wana dhamira yao kichwani," alisema Ofisa Mtendaji Mkuu huyo.

Kuhusu uchezeshaji, Kasongo alisema hadi kufikia raundi ya tano, waamuzi wengi wamejitahidi kuchezesha vizuri na hawajapokea malalamiko ya uchezeshaji mbaya.

"Naridhishwa na maamuzi ya waamuzi, si kwenye Ligi Kuu tu, hata kwenye Ligi ya Championship, ambako kulikuwa kunalalamikiwa sana, lakini ni raundi ya sita sasa, imekuwa tulivu bila vurugu wala malalamiko," alisema Kasongo.

## TGB yawatoa wasiwasi Watanzania kubashiri

**Na Maulid Mmbaga**

BODI ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania (TGB), imetoa wito kwa Watanzania kuwa na imani na mchezo wa kubahatisha unaoratibiwa na Kampuni ya Vodacom na kuwahakikishia kwamba unafuata sheria na kanuni za uendeshwaji wake.

Akizungumza jana wakati wa uzinduzi wa msimu mpya wa Vodacom Tusua Mapene uliofanyika Dar es Salaam, mwakilishi kutoka TGB, Rasuli Masudi, alisema michezo hiyo inasaidia kuinua kipato cha Watanzania pamoja na kutimiza ndoto zao.

"Niwaongeze imani Watanzania kwamba hii michezo inaratibiwa na Bodi ya Michezo ya Kubahatisha na wadau hawa wanakibali cha kuendesha shindano hilo, wanazingatia vigezo na masharti yote," alisisitiza Masudi.

Mkurugenzi wa Dijitali na Huduma za Ziada kutoka Vodacom, Nguvu Kamando, alisema awamu iliyopita iliwanufaisha Watanzania ya 400,000 walioshinda kwenye shindano hilo kwa kuwawezesha katika nyanja ya kiuchumi, biashara kilimo na vitendea kazi.

Alisema katika msimu mpya wa shindano hilo washindi watatu watapata magari mapya na mshindi wa jumla atajishindia Sh. milioni 300, na walifikia uamuzi wa kuanzisha msimu mpya wa kutokana na mabadiliko chanya waliyopata washindi wa msimu uliopita.

## Mahakama yatakiwa kufika Ligi Daraja la 1

**Na Hellen Mwango**

MTENDAJI Mkuu wa Mahakama ya Tanzania, Profesa Elisante Ole Gabriel, ameagiza uongozi wa michezo wa mhimili huo kufanya maandalizi mapema ili mashindano ya 2022 ya Shirikisho la Michezo ya Wizara na Idara za Serikali Tanzania (SHIMIWI), wapate ushindi zaidi na ikibidi wawe na timu Ligi Daraja la Kwanza.

Ole Gabriel alitoa rai hiyo jana jijini Dar es Salaam wakati akipokea vikombe ikiwamo hati ya ushindi wa nidhamu kwa jumla kwa timu za mahakama zilizoshiriki mashindano hayo yaliyomalizika Novemba 2, mwaka huu.

"Mahakama ni mhimili wa kutoa haki mmeonyesha mfano mzuri kwa kutenda haki na kuwapatia ushindi wa jumla wa nidhamu, maandalizi yaanze mara moja kwa ajili ya mashindano ya mwakani tukashinde kwa kishindo," alisema Prof. Ole Gabriel.

Akifafanua zaidi alisema wakifanya maandalizi mapema watafanya vema, hivyo wakajipange kwa mazoezi ikibidi wapande Ligi Daraja la Kwanza.

Naye Mkurugenzi wa Mipango na Ufuatiliaji, Erasmus Uiso, alisema mahakama ilipeleka kwaya ya mahakama, timu ya mpira wa miguu, mpira wa mikono (netball) timu za kuvuta kamba ya wanawake na wanaume.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### CITY YAMTAKA DE JONG
MANCHESTER City inaweza kuiomba Barcelona kuwapa kiungo wa Uholanzi, Frenkie de Jong mwenye umri wa miaka 24, kama miamba hao wa Hispania wakitaka kumsajili, Raheem Sterling mwenye umri wa miaka 26. **(El Nacional)**

### VLAHOVIC KUIKATAA ARSENAL
STRAIKA wa Fiorentina, Dusan Vlahovic anatarajiwa kukataa mpango wa kuhamia Arsenal Januari kwa sababu mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 raia wa Serbia, anasubiria ofa nyingine. **(Football Italia)**

### LAMPARD ATAJWA NORWICH
KOCHA wa zamani wa Chelsea, Frank Lampard, amefungua mazungumzo na Norwich City kuhusu kuwa kocha mpya pale Carrow Road. **(Football Insider)**

### ZIDANE HAENDI UNITED
NI ngumu kwa kocha wa zamani wa Real Madrid, Zinedine Zidane kuchukua nafasi ya ukocha kweye timu ya Manchester United kama klabu hiyo ya Old Trafford itamfukuza Ole Gunnar Solskjaer. **(AS)**

### FERNANDEZ HAMTAKI SOLSKJAER
KIUNGO wa Ureno, Bruno Fernandes mwenye umri wa miaka 27, ni mmoja wa wachezaji wakubwa wa Manchester United ambaye anahisi kwamba, kocha wao Ole Gunnar Solskjaer hafiti kuinoa timu hiyo. **(Mail)**

### GERRARD ATAKIWA VILLA
KLABU ya Aston Villa inaweza kumchukua Steven Gerrard kuwa kocha mpya baada ya kutimuliwa kwa Dean Smith. **(Telegraph)**


### MARTINEZ NAE ATAJWA
KOCHA wa Ubelgiji, Roberto Martinez anatajwa kuwania nafasi ya ukocha pale Aston Villa. **(Times)**

### RODGERS AIKATAA UNITED
KOCHA wa Leiceste City, Brendan Rodgers yupo tayari kuchukua mikoba ya Ole Gunnar pale Manchester United, ingawa angependa kusubiri hadi msimu ujao. **(Caught Offside)**

### TRAORE KUENDELEA KUCHEZA
KOCHA wa Wolves, Bruno Lage amesema kutokana na hali ya mkataba wa Adama Traore hakutamfannya kutomtumia winga huyo wa kimataifa wa Hispania mwenye umri wa miaka 25 ambaye mkataba wake umebaki miezi 18. **(Mail)**

### SANCHES ATAKIWA WOLVES
KLABU ya Wolves inamwania kiungo wa Lille na Ureno, Renato Sanches mwenye umri wa miaka 24 na wanaweza kumsajili wakati wa dirisha la Januari. **(Fichajes.net)**

### RAMOS KUBAKI PSG
MLINZI wa Hispania, Sergio Ramos mwenye umri wa miaka 35 hana mpango wa kuondoka Paris St-Germain, kwa mjibu wa kaka yake, Rene ambaye ni wakala wake. **(El Mundo, via Goal)**



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# ARTETA AMPINGA RANIERI, AWATETEA WACHEZAJI

**Kama ninatakiwa kuwaelezea ama timu yangu na klabu naweza kusema wote ni waungwana sana...**

**LONDON, England**

MIKEL Arteta amewaelezea wachezaji wake kuwa ni "waungwana sana" baada ya Claudio Ranieri kuwashutumua kwa kukosa heshima wakati Arsenal ikiibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Watford pale kwenye dimba la Emirates, Jumapili.

Kocha Mkuu wa Watford, Ranieri hakuwa na furaha kwa sababu wachezaji wa Arsenal hawakutoa mpira wakati wa majeruhi na ndio ilisababisha Emile Smith Rowe kufunga bao hilo pekee kwenye mchezo huo.

Matokeo hayo yamewafanya 'Washikabunduki' hao kufikisha mechi ya 10 bila kufungwa kwenye mashindano yote, huku Arteta akifikisha mechi 100 kama kocha wa Arsenal.

Arteta aliwatetea wachezaji wake baada ya tukio hilo, akibainisha kwamba, timu yake haikuwa na tatizo.

"Kama ninatakiwa kuwaelezea wachezaji wangu, timu yangu na klabu naweza kusema wote ni waungwana sana," alisema Arteta akiwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo huo.

"Lakini kama (Ranieri) anahisi kwamba timu yetu haikufanya kitendo cha kiungwana, timu yetu na naomba radhi kwa hilo, lakini kwa uhakika kabisa hatukutumia nafasi ile ili kupata bao."

Nahodha wa Arsenal, Pierre-Emerick Aubameyang, alikosa penalti yake ya pili mfululizo kwenye ligi, akiwa amekosa mbili tu kati ya 11 kwenye mashindano hayo, lakini Arteta bado ana imani na nyota wake huyo.

"(Aubameyang) ataendelea kupiga penalti kama atataka kufanya hivyo," aliongeza Arteta.








# XAVI KUANZA KUINOA BARCA LEO

**BARCELONA, Hispania**

XAVI ataanza kuinoa Barcelona kwenye mazoezi yake ya kwanza leo Jumanne, klabu hiyo imethibitisha.

Kiungo huyo wa zamani wa Barca alitangazwa kuwa kocha mpya wa kikosi hicho baada ya kufukuzwa kwa Ronald Koeman na jana Jumatatu alitambulishwa rasmi.

Xavi alirudi hapo 'Blaugrana' ambapo sasa wapo katikati ya msimamo kwenye LaLiga na amebainisha kwamba, mazoezi ya leo Jumanne yatakuwa ya nguvu.

Wakati huu kukiwa na mapumziko ya kupisha mechi za kimataifa, kiungo huyo gwiji ataanza kuiongoza timu hiyo ya Katalunya kwenye mchezo dhidi ya Espanyol, Jumamosi ya Novemba 20.

Wakati huo huo, Barcelona walitangaza kwamba, Eric Garcia na Nico Gonzalez waliumia kwenye mchezo wa Jumamosi ambao walitoka sare ya 3-3 na Celta Vigo.

Pia, Ansu Fati naye aliondoka uwanjani akiwa na maumivu ya nyama za paja kabla ya kipindi cha pili na anaendelea na matibabu.

# Shevchenko kocha mpya Genoa



**ROME, Italia**

KLABU ya Genoa ya nchini Italia, imemteua mchezaji wa zamani wa kimataifa wa Ukraine, Andriy Shevchenko kuwa kocha wao mkuu mpya, ilitangazwa juzi Jumapili.

Shevchenko alikuwa bila timu baada ya kujiuzulu kuinoa timu ya Taifa ya Ukraine ambayo ilifika robo fainali kwa mara ya kwanza kwenye michuano ya Euro 2020.

Gwiji huyo wa AC Milan, Shevchenko - amesaini mkataba utakaomweka kwenye timu hiyo hadi Juni 2024.

Genoa ipo kwenye mstari wa kushuka daraja na ilimtimua kocha wake, Davide Ballardini baada ya kutoka sare ya 2-2 na Empoli, Ijumaa.

Mchezo wa kwanza kwa Shevchenko kuiongoza Genoa utakuwa dhidi ya kikosi cha Jose Mourinho, AS Roma, Novemba 21, mwaka huu.

Shevchenko ambaye ameichezea Ukraine mechi 111, alishinda taji la Ligi Kuu Italia na Ligi ya Mabingwa Ulaya wakati wa kipindi cha miaka saba aliyokaa pale San Siro.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 45, alifunga mabao 173 pale Milan tangu alipojiunga na timu hiyo akitokea Dynamo Kiev mwaka 1999.

Shevchenko baadaye alijiunga na miamba ya Ligi Kuu England, Chelsea mwaka 2006 na alikuwa sehemu ya timu iliyoshinda taji la FA na EFL kabla ya kurudi tena Milan kwa mkopo mwaka 2008 na aliteuliwa kuwa kocha wa Ukraine mwaka 2016.

# 7,771,400

# JACKPOT
## MECHI WIKI HII

**BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13**

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 13/11/21 | 18:00 | Rochdale vs Leyton Orient | 2.27 | 3.28 | 2.99 |
| 02. 13/11/21 | 18:00 | Tranmere vs Sutton United | 2.32 | 3.23 | 2.94 |
| 03. 13/11/21 | 18:00 | Stevenage vs Mansfield | 2.46 | 3.20 | 2.76 |
| 04. 13/11/21 | 18:00 | Bristol Rovers vs Northampton | 2.41 | 3.19 | 2.85 |
| 05. 13/11/21 | 18:00 | Walsall vs Harrogate | 2.60 | 3.23 | 2.60 |
| 06. 13/11/21 | 18:00 | Altrincham vs Boreham Wood | 2.83 | 3.27 | 2.35 |
| 07. 13/11/21 | 18:00 | Yeovil vs Eastleigh | 2.38 | 3.22 | 2.83 |
| 08. 13/11/21 | 18:00 | Wealdstone vs Barnet | 2.43 | 3.41 | 2.63 |
| 09. 13/11/21 | 18:00 | Accrington vs Plymouth | 2.70 | 3.44 | 2.39 |
| 10. 13/11/21 | 20:15 | Mirandes vs Huesca | 2.34 | 3.14 | 2.99 |
| 11. 14/11/21 | 18:00 | UD Ibiza Eivissa vs Almeria | 3.13 | 3.18 | 2.24 |
| 12. 14/11/21 | 20:15 | Leganes vs Real Oviedo | 2.29 | 2.99 | 3.23 |
| 13. 14/11/21 | 20:15 | Burgos vs Ponferradina | 2.41 | 3.03 | 2.98 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

**JUMANNE - 09 - NOVEMBA 2021**

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 1277 | Gimpo Citizen vs Hwaseong FC | 1.56 | 3.62 | 5.41 |
| 14:00 | 2926 | Bangkok Utd vs BEC Tero Sasana | 1.37 | 4.72 | 6.36 |
| 15:00 | 5493 | Buriram Utd vs Nong Bua Pitchaya | 1.13 | 6.73 | 14.41 |
| 16:00 | 2458 | QPR U23 vs Ipswich U23 | 3.10 | 3.75 | 2.11 |
| 16:00 | 2915 | Peterborough United Reserve vs Sheffield United U23 | 3.65 | 3.90 | 1.89 |
| 16:00 | 3055 | Coventry U23 vs Crewe U23 | 1.32 | 5.60 | 8.20 |
| 21:30 | 1169 | Concordia Chiajna vs Astra Giurgiu | 1.48 | 3.80 | 6.16 |
| 22:00 | 1545 | Crewe vs Wolverhampton U21 | 2.24 | 3.62 | 2.65 |
| 22:00 | 2420 | Sunderland vs Bradford City | 1.67 | 4.00 | 4.70 |
| 22:00 | 3145 | Sheffield Wed vs Harrogate | 1.70 | 3.62 | 4.25 |
| 22:00 | 3375 | Stevenage vs Cambridge Utd | 2.93 | 3.41 | 2.15 |
| 22:00 | 3483 | Crawley Town vs Southampton U21 | 1.67 | 4.10 | 4.60 |
| 22:00 | 4053 | Wycombe vs Burton | 1.96 | 3.47 | 3.33 |
| 22:00 | 4230 | Morecambe vs Carlisle | 2.03 | 3.37 | 3.22 |
| 22:00 | 5014 | Leyton Orient vs Charlton | 2.56 | 3.38 | 2.42 |
| 22:00 | 5460 | Swindon Town vs Newport | 2.02 | 3.37 | 3.23 |
| 22:00 | 5677 | Scunthorpe vs Doncaster | 2.89 | 3.42 | 2.17 |
| 22:30 | 4248 | Stenhousemuir vs Albion Rovers | 2.28 | 3.17 | 2.89 |
| 22:45 | 1255 | Salisbury City vs Walton Casuals | 1.88 | 3.62 | 3.42 |
| 22:45 | 1350 | Royston Town vs Barwell | 1.58 | 4.05 | 4.53 |
| 22:45 | 1963 | Portsmouth vs Crystal Palace U21 | 2.50 | 3.42 | 2.45 |
| 22:45 | 2116 | Leatherhead vs Cheshunt | 5.01 | 4.04 | 1.53 |
| 22:45 | 2584 | Kings Langley vs Hartley Wintney | 2.51 | 3.48 | 2.41 |
| 22:45 | 2602 | East Thurrock vs Lewes | 5.78 | 4.72 | 1.40 |
| 22:45 | 2789 | Hungerford Town vs Hemel Hempstead | 1.89 | 3.56 | 3.46 |
| 22:45 | 2868 | Brackley Town vs Spennymoor Town | 2.19 | 3.42 | 2.85 |
| 22:45 | 2941 | Merstham vs Cray Wanderers | 2.29 | 3.51 | 2.64 |
| 22:45 | 3008 | Bowers Pitsea vs Corinthian Casuals | 2.50 | 3.45 | 2.65 |
| 22:45 | 3048 | Aldershot vs Wrexham | 3.66 | 3.22 | 1.99 |
| 22:45 | 3191 | Metropolitan Police vs Chesham Utd | 1.77 | 3.66 | 3.81 |
| 22:45 | 3283 | Newtown AFC vs Bala Town | 2.99 | 3.42 | 2.11 |
| 22:45 | 3842 | Fleetwood Town vs Accrington | 2.14 | 3.36 | 2.98 |
| 22:45 | 3963 | Ipswich vs Colchester | 1.52 | 3.86 | 5.40 |
| 22:45 | 3989 | Buxton FC vs Atherton Collieries | 1.50 | 4.90 | 5.40 |
| 22:45 | 4275 | Hednesford Town vs Stratford Town | 2.11 | 3.62 | 2.85 |
| 22:45 | 4473 | Sutton United vs AFC Wimbledon | 2.66 | 3.33 | 2.36 |
| 22:45 | 4503 | Banbury United vs Rushall Olympic | 1.85 | 3.72 | 3.43 |
| 22:45 | 4590 | Mansfield vs Newcastle U21 | 2.02 | 3.46 | 3.17 |
| 22:45 | 4674 | Ashton Utd vs Radcliffe Borough | 2.38 | 3.38 | 2.60 |
| 22:45 | 4805 | St Ives Town vs Redditch United | 2.56 | 3.53 | 2.35 |
| 22:45 | 4809 | AFC Hornchurch vs Haringey Borough | 1.83 | 3.75 | 4.10 |
| 22:45 | 5123 | Poole Town vs Weston Super Mare | 1.65 | 3.86 | 4.25 |
| 22:45 | 5235 | Penybont vs Cardiff Met Uni. | 2.42 | 3.38 | 2.56 |
| 22:45 | 5296 | Leamington vs York City | 3.32 | 3.51 | 1.94 |
| 22:45 | 5309 | Bromsgrove Rovers vs Tamworth | 2.70 | 3.52 | 2.24 |
| 22:45 | 5489 | Barrow vs Leicester City U21 | 2.21 | 3.47 | 2.79 |
| 22:45 | 5581 | Haverfordwest vs Barry Town FC | 2.12 | 3.53 | 2.90 |
| 22:45 | 5675 | Whitby Town vs Utd of Manchester | 2.30 | 3.45 | 3.00 |
| 22:45 | 5681 | Farnborough Town vs Beaconsfield Sycob | 1.36 | 4.82 | 6.36 |
| 22:45 | 5846 | Merthyr Town vs Dorchester Town | 2.21 | 3.46 | 2.79 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# RAMOS HAONDOKI PSG



**PARIS, Ufaransa**

SERGIO Ramos hana mpango wa kuondoka Paris Saint-Germain na kwa sasa amejikita kujiandaa kucheza mchezo wake wa kwanza na klabu hiyo haraka inavyowezekana, kwa mujibu wa wakala wake.

Ramos bado haijacheza mchezo wowote kwa PSG tangu alipojiunga kwa uhamisho huru kutoka Real Madrid, ambako alikaa kwa misimu 16.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 35, aliumia kigimbi mwishoni mwa Julai na kumfanya kuwa benchi, huku pia akikosa sehemu kubwa ya msimu wa 2020-21.

Msimu uliopita alianza katika mechi 15 za La-Liga zikiwa chache zaidi ukilinganisha na mechi 35 alizoanza msimu mwingine kabla.

Amecheza mechi tano tu kwenye mashindano yote kwa klabu hiyo mwaka 2021, sawa na dakika 395 dimbani, huku mara ya mwisho kuichezea timu ya Taifa ya Hispania ni dhidi ya Kosovo, Machi mwaka huu.

Kuumia kwa Ramos kumefanya asipate nafasi ya kuichezea timu yake mpya ya PSG na kukawa na ripoti kwamba klabu hiyo inafikiria kusitisha mkataba na mlinzi huyo wa kati.

Hata hivyo, miamba hao wa Ligue 1 walitangaza Ijumaa kwamba, Ramos anajiandaa kuanza mazoezi wiki hii na wakala wake amebainisha wazi kwamba, haondoki hapo kwenye dimba la Parc des Princes.

"Sergio atacheza haraka hivi karibuni," alisema kaka wa Ramos, Rene ambaye ni wakala wake akinukuliwa na Mundo Deportivo.

"Ataendelea kuwapo PSG na hakuna mpango wowote wa kuondoka kwa sasa, hilo halina shaka kabisa."


# Maguire: Man United ipo kwenye hali mbaya

**MANCHESTER, England**

HARRY Maguire amesema kiwango cha sasa cha Manchester United "hakipo sawa" baada ya kufungwa na Manchester City, Jumamosi.

Kikosi cha Pep Guardiola kilipata ushindi huo pale kwenye dimba la Old Trafford kwa mabao ya Eric Bailly alieyejifunga na lile la Bernardo Silva na kuwafanya kuibuka na ushindi wa 2-0.

Ole Gunnar Solskjaer alikuwa na rekodi nzuri dhidi ya Guardiola katika mechi zilizopita, lakini United walipiga shuti moja tu na kilikuwa kipigo chake cha nne msimu huu kati ya mechi sita zilizopita.



'Mashetani Wekundu' hao wameruhusu mabao 11, kwenye mechi sita za ligi nyumbani msimu huu kwa mara ya kwanza tangu msimu wa 1976-77.

Naye Maguire amekuwa hayupo kwenye kiwango bora kuanzia katika kichapo cha mabao 5-0, walichokipata kutoka kwa Liverpool Oktoba 24, mwaka huu.

Katika twitter yake aliyoiposti Jumapili, Maguire alisema kwamba, anatambua kiwango cha timu hiyo hakipo sawa, lakini alisisitiza United watarudi kwenye ubora wao.

"Kama kundi la wachezaji tunapitia kwenye wakati mgumu sana," aliandika Maguire.

"Lakini naamini kwamba, tutarudi kwenye kiwango chetu kwani hiki ni kipindi cha mpito tu kwa sasa.

"Tunajua na tunakubali kwamba hatupo kwenye kiwango chetu. Tupo kwenye wakati mgumu sana."

Michezo

Jumanne Novemba 9 , 2021

Nipashe



## Arteta ampinga Ranieri, awatetea wachezaji

UKURASA 21

**NA WAJE TU...**



Wachezaji wa Taifa Stars, wakiwa mazoezini katika Uwanja wa Benjamin Mkapa jana, wakijiandaa na mchezo dhidi ya DR Congo utakaopigwa uwanjani hapo Alhamisi, kuwania kufuzu fainali za Kombe la Dunia zitakazofanyika mwakani nchini Qatar. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# YANGA YAFUATA 'UBANI' KWA MLANDEGE, KMKM

●●●Kushusha mastaa wake Uwanja wa Amaan Zanzibar leo usiku, Nabi aanika anachokitaka...

**Saada Akida, DAR na Hawa Abdallah, Z'BAR**

WAKATI kikosi kikijiandaa kuikabili Namungo FC, kikosi cha Yanga kinaondoka Dar es Salaam leo kuelekea visiwani Zanzibar kwa maandalizi zaidi na kikiwa huko kitacheza mechi mbili za kirafiki dhidi ya Mlandege na KMKM FC, kabla ya kurejea tayari kwa mchezo huo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kwa mujibu wa Meneja wa Yanga, Hafidh Saleh, baada ya mapumziko ya siku moja waliyopewa wachezaji ambao hawako katika majukumu ya timu zao za taifa, yalimalizika jana, Jumatatu na kuanza mazoezi kabla ya baadaye leo kusafiri kuelekea visiwani Zanzibar kwa ajili ya kambi fupi na kucheza mechi hizo mbili za kirafiki.

"Ni kweli tumepata mwaliko wa kwenda Zanzibar na ratiba iliyokuwapo ni kucheza mechi mbili za kirafiki, kuhusu timu bado hatujaambiwa, ila wachezaji watakaoondoka ni wale wote ambao wako fiti na hawana majukumu katika timu zao za taifa," alisema meneja huyo.

Alisema mechi hizo zitasaidia benchi lao la ufundi kupata mwanga wa kuendelea kuimarisha kikosi chao kuelekea katika michezo yao ijayo ya Ligi Kuu ambayo imekuwa na ushindani mkubwa.

Kwa upande wa mratibu wa mechi hizo kutoka Zanzibar, Idd Juma, alisema Yanga watakaa siku tatu visiwani humu kuanzia leo usiku ambapo watacheza mechi ya kwanza dhidi ya Mlandege na ya pili itakuwa Ijumaa wiki hii dhidi ya KMKM, michezo yote itapigwa katika Uwanja wa Amaan.

Naye Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, alisema ameanza kuwapa mbinu mpya wachezaji wake ili kuweza kukabiliana na timu zenye tabia ya kucheza kwa kuzuia muda wote maarufu kama 'kupaki basi'.

Alisema anatambua ligi msimu huu imekuwa na ushindani na kila timu inaingia kwa mbinu zake, lakini amepata bahati ya kuwaona Namungo FC wanavyocheza kwa kuzuia na sasa anafanyia kazi ubora na udhaifu wa wapinzani wao.

Alisema licha ya kuwapo kwa wachezaji pungufu, wengi wao wakiwa kwenye majukumu ya timu zao za taifa, ana lazimika kuendelea na mazoezi huku akiwapa mbinu za kiufundi wachezaji walikuwapo ikiwamo kuwaweka fiti kabla ya wenzao kurejea na kuungana nao kwa mechi hiyo dhidi ya Namungo na zinginezo.


"Wakati huu tukiwa tumepisha mechi za Kalenda ya Fifa, nitakuwa na kazi kubwa ya kukisuka kikosi hasa safu ya ushambuliaji kuwa makini kwenye nafasi wanazopata, kupambana na timu ambazo zinacheza kwa kuzuia muda mwingi," alisema Nabi.

Alisema licha ya kupata matokeo mazuri katika michezo waliyocheza, bado anahitaji kujiimarisha zaidi na kuhakikisha wanapambana kutafuta matokeo katika kila mchezo wa ligi hiyo.

"Ligi msimu huu imekuwa ya ushindani mkubwa, tunahitaji kupambana kutumia mbinu na ufundi ili kuwazidi wapinzani wetu kuweza kupata matokeo mazuri na kufikia malengo," alisema kocha huyo.

Yanga itawakabili Namungo katika mchezo ujao wa Ligi Kuu Bara, utakaopigwa Novemba 20, mwaka huu, katika Uwanja wa Ilulu mkoani Lindi.

## Xavi kuanza kazi Barca leo



**BARCELONA, Hispania**

XAVI ataanza kuinoa Barcelona kwenye mazoezi yake ya kwanza leo Jumanne, klabu hiyo imethibitisha.

UK. 22

## Viongozi Ligi Kuu someni kanuni - TPLB



**Na Adam Fungamwango**

BODI ya Ligi nchini (TPLB), imesema imebaini kuwa viongozi wengi wa klabu nchini hawasomi au kuzipitia kanuni, hivyo kuwasababishia wao na klabu zao kupata matatizo mengi ya kufungiwa au kulipishwa faini.

UK. 20

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >